MAANA ZA KIMUKTADHA ZILIZOJITOKEZA KATIKA SEMI ZILIZOANDIKWA KATIKA KANGA

AMINA MAKAME HAJI

TASINIFU HII IMETOLEWA KWA MADHUMUNI YA KUTOSHELEZA BAADHI YA MASHARITI YA SHAHADA YA UZAMILI (M.A KISWAHILI-ISIMU) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA

2019

IDHINI

Aliyetia sahihi hapo chini anadhibitisha kuwa ameisoma kazi hii na anapendekeza kuwa Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kukubali kupokea tasnifu hii: **Maana za kimuktadha zilizojitokeza katika semi zilizoandikwa katika majina ya kanga**, katika kukamilisha baadhi ya matakwa ya shahada ya uzamili Kiswahili Isimu ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

Mw. Bakari Kombo

(Sahihi)

Tarehe

HAKIMILIKI

Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa namna yoyote sehemu yoyote ile ya tasinifu hii kwa njia yoyote kama vile, kielektroniki, kurudufu nakala, kurekodi au njia yoyote nyingine bila ya idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba.

TAMKO

Mimi, **Amina Makame Haji** natamka kuwa kazi hii ni yangu mwenyewe haijatolewa na haitotolewa kwa mahitaji ya kutunukiwa shahada ya uzamili au shahada nyingine ambayo ni sawa au karibu sawa na hii katika chuo kikuu chengine.

Sahihi

Tarehe

TABARUKU

Natabaruku kazi hii kwa mama yangu mpenzi MIZA CHUMU MAKAME kwa upendo wake wa dhati aliokuwanao kwangu tangu utotoni hadi sasa. Aidha, naitabaruku kazi hii kwa baba yangu MAKAME HAJI GOGO. Pia kwa mume wangu kipenzi ALI SHARIF OTHMAN na ndugu zangu HIDAYA, HASNUU na CHUMU kwa kuniunga mkono na kuniauni muda wote wa masomo. Mwisho kwa watoto wangu wapenzi AJMAL na AHSAN.

SHUKURANI

Kwa kuanzia ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uzima na kunipa uwezo wa kukamilisha utafiti huu. Kwa kiasi kikubwa ukamilishaji wa utafiti huu umetokana na msaada wa watu wengi. Nitakuwa mwizi wa fadhila endapo nitashindwa kuwashukuru watu ambao wamechangia ukamilishaji wa kazi hii.

Hatahivyo haitakuwa rahisi kuwataja wote kwa majina kwa sababu ni wengi, ninawashukuru wote nitakao wataja na wale nisiowataja waliochangia kufanikisha kazi hii kwa njia yoyote. Ninatoa shukurani zangu kwa msimamizi wangu wa utafiti, Mw. Bakari Kombo kwa kukubali kuwa msimamizi wangu na kulisimamia pendekezo langu la utafiti na kunielekeza, kunishauri na kunikosoa katika kipindi chote cha utafiti huu pamoja na majukumu mengi aliyonayo. Ametumia busara na uvumilivu mkubwa hadi kufikia hatua ya kukamilika kazi hii. Vilevile ninawashukuru walimu wangu, wahadhiri wa Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kwa kunifundisha kozi ya mbinu za utafiti ambayo iliniongoza katika uchambuzi wa data nilizozikusanya. Aidha, ninatoa shukurani kwa Dkt. Hadija Jilala, Dkt. Zelda Elisifa na Dkt. Ligembe kwa kunifundisha kozi ya Semantiki, mofolojia na fonolojia ambazo zilinisaidia katika utafiti wangu. Pia sitowasahau Bi Aisha Ameir kwa msaada wake mkubwa alionipatia.

Mwisho ninaishukuru familia yangu akiwemo Mume wangu bwana Ali Sharif Othman na watoto wangu wote kwa uvimilivu mkubwa waliouonesha wakati nikiwa katika shughuli za utafiti huu.

IKISIRI

Mada ya utafiti huu ilikuwa ni kuchunguza Maana za Kimuktadha zilizojitokeza katika Semi

zilizoandikwa katika Majina ya Kanga. Utafiti huu ulikuwa na malengo matatu ya msingi. Malengo hayo ni Kubainisha semi mbali mbali zilizoandikwa katika kanga kutegemeana na maudhui zake. Kubainisha maana za semi teule zilizoandikwa kwenye kanga kwa kuangalia maana ya msamiati na muktadha na Kuchambua maana za muktadha ya semi teule zilizoandikwa

kwenye kanga. Mbinu za kukusanyia data za utafiti huu zilkuwa ni mahojiano na uchunguzi makini. Uchambuzi wa data ulifanyika kwa mkabala wa kimaelezo huku ukiongozwa na nadharia tatu. Nadharia hizo ni Maana Kimatumizi, Maana Kimuktadha na nadharia ya Simiotiki. Matokeo ya utafiti huu yalionesha kuwa kuna semi mbalimbali zilizotofautiana kimaudhui ambazo zimeandikwa katika kanga. Semi hizo zimejikita katika maudhui ya mila na utamaduni wa jamii, dini na imani, maarifa mengineyo, bidii katika kazi na subirá na uvumilivu. Kwenye lengo la pili, matokeo yalionesha kuwa maana za semi zinajikita kimsamiati na kimuktdha. Maana za kimsamiati huibuka kutokana na vijenzi mahususi vilivyojenga usemi wenyewe. Maana za kimuktadha zinatokana na tafsiri mahususi inayotokana na mtazamo na muktadha wa kimatumizi kama inavyofahamika na jamii husika. Na katika lengo la tatu amegundua kuwa semi zilizo katika maudhui mbalimbali huandikwa kwenye kanga ili kufikisha ujumbe maalum kwenye jamii ambapo kanga huvaliwa. Semi hizo kukanya, hukosoa na hata kuelekeza juu ya utendaji bora wa mambo katika jamii husika. Kwa mfano maswali ya wivu uliokomaa ulizungumziwa, umuhimu wa kubaki kwenye ndoa, umuhimu wa kuheshimiana, umuhimu wa bidii ya kazi, subirá na uvumilivu na maadili kadha ya kijamii yalihusishwa kwenye lengo hili la tatu.

YALIOMO

IDHINI ii

HAKIMILIKI iii

TAMKO iv

TABARUKU v

SHUKURANI vi

ORODHA YA MAJEDWALI xii

IKISIRI vii

YALIOMO viii

SURA YA KWANZA: UTANGULIZI WA JUMLA 1

1.0 Utangulizi 1

1.1 Usuli wa Tatizo la Utafiti 1

1.2 Tatizo la Utafiti 2

1.3 Malengo ya Utafiti 3

1. 3.1 Lengo Kuu 3

1.3.2 Malengo Mahususi 4

1.4 Maswali ya Utafiti 4

1.5 Umuhimu wa Utafiti 4

1.6 Mipaka ya Utafiti 5

1.7 Hitimisho 5

SURA YA PILI: MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA 6

2.1 Utangulizi 6

2.2 Mapitio ya Tafiti kuhusu Semi 6

2.2.1 Dhana ya Semi 6

2.2.2 Kazi Tangulizi kuhusu Semi 11

2.3 Kiunzi cha Nadharia 16

2.4 Maana ya Nadharia 16

2.4.1 Nadharia ya Maana ya Matumizi 17

2.4.2 Nadharia ya Maana Kimuktadha 19

SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI 23

3.1 Utangulizi 23

3.2 Eneo la Utafiti 23

3.2.1 Usampulishaji 24

3.2.2 Sampuli 24

3.3 Mkabala wa Uchambuzi wa Data 25

3.4 Njia za Ukusanyaji wa Data 26

3.4.1 Mahojiano (Usaili) 26

3.4.2 Uchunguzi Makini 26

3.5 Mkabala wa Uchambuzi wa Data 27

3.6 Hitimisho 27

SURA YA NNE: UCHAMBUZI NA UWASILISHAJI WA DATA 28

4.1 Utangulizi 28

4.2 Utafiti na Malengo yake 28

4.2.1 Kubainisha Semi Mbali mbali zilizoandikwa katika Kanga 29

4.2.1.1 Semi zilizoandikwa katika Kanga zenye kuhusu Mila na Utamaduni wa Jamii 30
4.2.1.2 Semi zilizoandikwa katika Kanga zenye Uhusiano wa Dini na Imani 31
4.2.1.3 Semi zilizoandikwa katika Kanga zinazohusu Maarifa Mengineyo 32
4.2.1.4 Semi zilizoandikwa katika kanga zinazohusu Bidii katika Kazi 32
4.2.1.5 Semi Zinazohusu Subira na Uvumilivu 33
4.2.1.6 Semi Zilizoandikwa katika Kangazinazohusu Ushirikiano 34
4.2.2 Uainishaji wa Maana za Kimsamiati na Muktadha wa Semi Teule 34
4.2.2.1 Semi zilizoandikwa kwenye kanga zenye kuhusu Mila na Utamaduni wa Jamii 34
4.2.2.2 Semi Teule zilizoandikwa kwenye Vazi la Kanga zenye Uhusiano wa Dini na Imani 36
4.2.2.3 Semi zilizoandikwa katika majina ya kanga Zinazohusu Bidii katika Kazi 37
4.2.2.4 Semi Zinazohusu Subira na Uvumilivu 38
4.2.2.5 Semi zilizoandikwa kwenye Kanga zinazohusu Ushirikiano 40
4.3 Kimuktadha zinavyodhihiri kwenye Semi zenye Maudhui Mbalimbali 41
4.3.1 Maana za Kimuktadha zinavyodhihiri kwenye Semi zenye Maudhui ya Utamaduni 41
4.3.2 Maana za Kimuktadha zinavyodhihiri kwenye Semi zenye Maudhui ya Imani na Dini 47
4.3.3 Maana za Kimuktadha zinavyodhihiri kwenye Semi zenye Maudhui zinazohusiana na Maarifa Mbali Mbali 51

4.3.4 Maana za Kimuktadha zinavyodhihiri kwenye Semi zenye Maudhui zinazohusiana na Bidii katika Kazi 52

4.3.5 Maana za Kimuktadha zinavyodhihiri kwenye Semi zenye Maudhui zinazohusiana na Subira na Uvumilivu 54

4.3.6 Maana za Kimuktadha zinavyodhihiri kwenye Semi zenye Maudhui ya Ushirikiano 55

4.4 Hitimkisho 56

SURA YATANO: MUHTASARI WA UTAFITI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO 57

5.1 Utangulizi 57

5.2 Muhtasari 57

5.2.1 Lengo Mahsusi La Kwanza 58

5.2.2 Lengo Mahsusi la Pili 58

5.2.3 Lengo Mahsusi la Tatu 59

5.3 Hitimisho 59

5.3.1 Utoshelevu wa Nadharia 59

5.4 Mapendekezo ya Utafiti 60

5.4.1 Mapendekezo kwa Tafiti Zijazo 61

MAREJELEO 62

VIAMBATANISHO 66

ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali na 1 : Idadi ya Sampuli 25

Jedwali na. 2: Semi zilizoandikwa kwenye kanga zenye kuhusu Mila na Utamaduni wa Jamii 35

Jedwali na. 3: Semi zilizoandikwa kwenye kanga zenye kuhusu Dini na Imani . 36

Jedwali na. 4: Semi zilizoandikwa kwenye kanga zenye kuhusu Bidii katika Kazi 37

Jedwali na. 5: Semi zilizoandikwa katika majina ya kanga zinazohusu Maarifa Mengineyo 38

Jedwali na. 6: Semi zilizoandikwa kwenye kanga zenye kuhusu Uvumilivu 39

Jedwali na. 7: Semi zilizoandikwa kwenye kanga zenye kuhusu Ushirikiano..... 40

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI WA JUMLA

1.0 Utangulizi

Sura hii inatoa utangulizi wa jumla kuhusu utafiti unaochunguza Maana za Kimuktadha zilizojitokeza katika semi zilizoandikwa katika majina ya Kanga. Katika sura hii mjadala utajikita kwenye usuli wa tatizo, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti, eneo la utafiti, na muundo wa tasnifu.

1.1 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Kila jamii ina mfumo wake wa maisha yanayoendelea siku hadi siku yanayojengwa na mila, desturi, imani, itikadi, utamaduni na kadhalika. Wanajamii hujaribu kutumia semi zilizoandikwa katika majina ya kanga kama ni njia moja wapo ya kufikishia ujumbe katika jamii husika.Maana hizo zinawezekana kuwa ni za moja kwa moja au za kimuktadha. Kwa hakika semi ni muhimu sana miongoni mwa vipengele vya fasihi ya jamii. Semi za jamii husika huakisi hali halisi ya maisha ya jamii hiyo. Wataalamu mbalimbali wamefanya utafiti kuhusu semi. Miongoni mwa wataalamu hao ni pamoja na Balisidya (1979), TUMI (1990), Mbunda (1992), Mulokozi, (1998), Senkoro (2011) na Kiiza (2004). Katika tafiti zao wataalamu hawa wana maoni yanayofanana na kwa jumla wanafasili kwamba, “semi ni fungu la tungo la fasihi simulizi ambazo ni fupi zenye kutumia picha tamathali za semi na ishara”. Watafiti hawa katika tafiti zao inaonesha kuwa wameshughulikia zaidi methali, vitendawili, nahau na misemo. Mtafiti wa utafiti huu amekusudia kuchunguza maana za muktadha zilizojitokeza katika semi zilizoandikwa katika majina ya kanga.

1.2 Tatizo la Utafiti

Mtafiti wa mada hii ameona wazi kuwa kuna tafiti nyingi zilizokwishafanywa juu ya mada ya semi katika vipengele tofauti. Kwa mfano Mahenge (2009) alichunguza zilizoandikwa katika kuta za vyoo zina utajiri mkubwa wa matumizi ya lugha ya kitamathali semi zilizoandikwa kwenye tiketi za daladala jijini Dar es salaam. Katika utafiti wake aliangalia kipengele cha fani na maudhui na kugundua kuwa baadhi ya semi zilikuwa ni methali na nyengine ni maneno ya kawaida. Migodella (2011) alichunguza ufasihi wa misemo au semi ziliziandikwa katika sehemu za umma, akitolea mifano misemo iliyoandikwa katika kuta za vyoo. Matokeo ya utafiti wake yanaonyesha kwamba semi kama vile tashbiha, tafsida, sitiari, taswira, ishara, picha nakadhalika. Uledi (2012) nae alichunguza muundo wa vipengele vya lugha katika methali na vitendawili kwa jamii ya Wamakunduchi. Kazi yake ilikuwa ni kulinganisha semi hizo na zile za Kiswahili Sanifu. Katika utafiti wake aligundua kuwa katika kila methali na vitendawili kuna vipengele mbali mbali vya lugha vinavyotumika katika ujenzi wake. Hassan (2013) alichunguza dhima za methali katika jamii ya Wapemba na kubaini kwamba methali zinatumika katika jamii ya Wapemba kwa kuangalia dhima ya methali ili kudumisha dhamira na maadili katika jamii.Vile vile Alhabib (2012) alichunguza matumizi ya taswira katika nyimbo za taarab na kugundua kuwa kipengele cha misemo kinajidhihirisha katika nyimbo za taarab. Vile vile Rajab (2012) alifanya utafiti juu ya dhima za misemo iliyoandikwa katika fulana, ambapo alishughulikia zaidi kipengele cha dhamira na matumizi ya lugha katika jiji la Dar es salaam. AIichogundua ni kwamba maandishi yaliyoandikwa katika vazi la fulana yamejaa dhamira mbali mbali. alitaja baadhi ya dhamira hizo kuwa ni umaskini, hali ngumu ya maisha, UKIMWI, dini, elimu, chuki,

maisha, wivu, pesa, umuhimu wa kufanya kazi pamoja na vita dhidi ya magonjwa. Juma (2016) akafanya utafiti juu ya kuchunguza fani na dhamira za semi zilizoandikwa katika vyombo vya safari vya baharini kisiwani Pemba. Katika kazi yake hiyo aligundua kuwa katika semi zilizoandikwa katika vyombo vya safari zimetumika mbinu mbali mbali za kisanaa kama vile tashtiti, taswira, kejeli, methali, misemo, simo, misimu na kadhalika. Vile vile aligundua kuwa dhamira inayotumika katika semi hizo ni dhamira ya maisha ya kila siku pamoja na maisha ya baadae huko akhera. Dhamira hizo ziliwasilishwa na kujitokeza katika semi zilizoandikwa katika vyombo vya baharini kisiwani Pemba.

Tafiti zote zinazohusu semi zilizofanywa na watafiti walioitangulia kazi hii, kwa kiasi anachoelewa mtafiti hakuna kazi yoyote inayochunguza maana za muktadha zilizojitokeza katika semi zilizoandikwa katika majina ya kanga. Hili ni pengo lililo wazi linalopaswa kuzibwa. Hivyo basi, mtafiti wa kazi hii ameona ipo haja ya kuchambua maana za muktadha zilizojitokeza katika semi zilizoandikwa katika majina ya kanga ili kuziba pengo lililoachwa na watafitii waliomtangulia.

1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu umeongozwa na malengo yafuatayo:-

1. 3.1 Lengo Kuu

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza maana za muktadha zilizojitokeza katika semi zilizoandikwa katika kanga kisiwani Pemba

1.3.2 Malengo Mahususi

Utafiti huu utajumuisha malengo mahsusi yafuatayo :-

i. Kubainisha semi mbali mbali zilizoandikwa katika kanga zivaliwazo kisiwani Pemba kutegemeana na maudhui zake.

ii. Kubainisha maana za semi teule zilizoandikwa kwenye kanga kwa kuangalia maana ya msamiati na muktadha

iii. Kuchambua maana za muktadha ya semi teule zilizoandikwa kwenye kanga

1.4 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu una jumla ya maswali matatu ambayo yatamuongoza mtafiti kukamilisha malengo yote ya utafiti. Maswali hayo ni kama yafuatayo:-

i. Ni semi gani ambazo hujitokeza katika majina ya kanga?

ii. Ni maana zipi za kimsamiati hupatikana katika semi teule zilizoandikwa katika kanga?

iii. Ni zipi maana za kimuktadha zinazopatikana katika semi teule zilizoandikwa kwenye kanga kisiwani Pemba?

1.5 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu baada ya kukamilika kwake utakuwa na umuhimu mkubwa katika nyanja mbalimbali. Kitaaluma utafiti huu utaweza kutumika kama ni chanzo cha taaluma kitakachoelekeza namna ambavyo semi zilizoandikwa katika kanga jinsi gani zinavyojitokeza maana zake za kimuktadha.

Vilevile, utafiti huu utasidia katika kuhifadhi na kurithisha mila na desturi za jamii na historia ya jamii kwa manufaa ya kizazi kijacho. Utafiti huu pia unaweza kutumika kama marejeleo ya kufanya tafiti nyingine katika isimu. Aidha, mapendekezo yatakayotolewa katika utafiti huu juu ya tafiti zijazo katika maeneo ambayo utafiti huu haukuweza kuyagusa kutokana na kujitenga na malengo mahsusi ya utafiti huu, yatasaidia kuwapa mwongozo watafiti wengine kuibua tafiti zaidi katika taaluma ya isimu.

1.6 Mipaka ya Utafiti

Hakuna marefu yasiyokuwa na mwisho wake, na ndio maana mtafiti wa kazi hii akaamua kulenga kazi yake katika kuchunguza maana za muktadha zilizojitokeza katika semi zilizoandikwa katika majina ya kanga na wala sio kuchunguza maana za muktadha zilizoandikwa katika vyanzo vyengine vya semi za lugha ya Kiswahili kama vile katika vyombo vya usafiri, kwenye makawa, kuta majengo tofauti na katika maeneo mengine.

1.7 Hitimisho

Sura hii ni sura ya utangulizi ambayo imejadili juu ya vipengele mbalimbali vya utangulizi kama vile usuli wa utafiti, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti na mipaka ya utafiti.

SURA YA PILI

MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA

2.1 Utangulizi

Sura hii inaonesha mapitio ya maandishi mbalimbali ya wataalamu. Kupitia kazi tangulizi, ni kitendo cha kuchunguza kwa kina kazi ambazo zimeandikwa hasa zile zenye uhusiano na mada inayofanyiwa utafiti. Mapitio ya kazi tangulizi ni mpangilio maalumu na ufafanuzi wa uchambuzi wa maandishi kuhusu habari inayohusiana na suala la utafiti Enon (1998:41). Kazi tangulizi zinaweza kuwa ni vitabu, makala, majarida mbalimbali na vyanzo vyengine vinavyotoa muongozo kwa mtafiti kuweza kugundua pengo ambalo linahitajika.

2.2 Mapitio ya Tafiti kuhusu Semi

Katika sehemu hii mtafiti ameonesha dhana ya semi kama zilivyotolewa na wataalamu mbalimbali.

2.2.1 Dhana ya Semi

Kwa kuwa utafiti huu unahusu semi, mtafiti amehisi ipo haja ya kufafanua dhana hii. Wataalamu walioongelea kuhusu semi ni pamoja na Finnegan (1979), Balisidya (1979), Ngolena Honero (1982), Mbunda (1992), Mulokozi (1996), na Wamitila (2003:135) ambao wote kwa pamoja wanakubaliana kwamba, Semi ni utanzu miongoni mwa tanzu za fasihi simulizi. Wataalamu hao wamezifasili semi kwa kusema kuwa semi ni kauli au tungo fupifupi zinazobeba misemo pamoja na mafumbo yanayosababisha kupatikana kwa mafunzo katika jamii. Kupitia Kuhusu mgawanyo wa semi wataalamu hawa wametofautiana katika kuziainisha semi. Mulokozi (1996) amegawanya semi kuwa ni methali, mafumbo, vitendawili, misimu,

lakabu pamoja na kauli tauria. Balisidya (keshatajwa) amezigawa semi katika makundi matatu nayo ni methali, misimu na vitendawili. Baadae aligawa semi kwenye vipera vidogovidogo ndani yake., Mfano katika methali; kuna misemo na nahau na katika vitendawili kuna mafumbo na vitendawili. Ngole na Honero (1982) Wameeleza vigezo ambavyo vinatofautisha misemo na methali. Kigezo kimoja kinachotumika kutofautisha misemo ni uzito wa agizo au adili anayolipata binaadamu. Usemi ambao hautoi agizo au adili maalumu unaitwa misemo na ule ambao unatoa agizo au adili kwa binadamu unaitwa methali.

Kwa kawaida inaoneshea kuwa semi katika lugha ya Kiswahili zinatumia picha mbalimbali kama vile mimea, ndege, wanyama na viumbe vyenginevyo. Picha hizi huwekwa kwa lengo la kumwakilisha mwanaadamu. Semi ni kielelezo cha dhamira ya Mswahili, inamvutia na kumpendeza mtu hadi anafahamu na kuelewa dhamira ya usemi huo ili kupata maana yake iliyotumika pamoja na ujumbe uliokusudiwa.

Mlacha (1985) ameielezea semi katika kipera cha methali kuwa ni sentensi yenye sura kama methali yenye muundo wa kipekee, ambao husaidia kutofautisha methali na sentensi nyingine. Methali ni fupi na zimekamata matendo mapana sana yanayoweza kufafanulika kwa maneno ya kawaida. Balisidya (ameshatajwa) amegawanya fasihi simulizi katika tanzu tatu nazo ni nathari, ushairi na semi. Katika kipengele cha semi yeye ameona kuwa zimegawika katika vitendawili, mafumbo, methali, misemo, nahau na misimu. Katika utafiti wake yeye alijishughulisha na kuchunguza chimbuko la matambiko ya uchawi na dini. Mulokozi (keshatajwa) ameainisha tanzu za semi kuwa ni methali, vitendawili, misimu, mafumbo na lakabu. Ameendelea kusema kuwa methali ni semi fupi fupi zenye kueleza kwa muhtasari

fikra au mafunzo mazito yaliyotokana na uzoefu wa jamii. Mulokozi (keshatajwa) ameainisha tanzu hii kwa kutumia kigezo cha umbile na tabia ya kazi inayohusika. Katika kigezo hiki ameonesha matumizi ya lugha, mfano methali hutumia tamathali, sitiari na mafumbo. Ametolea mfano methali isemayo“*haraka haraka haina baraka*”. Katika utafiti wake ameeleza vitendawili ni usemi uliofumbwa ambao hutolewa kwa hadhira ili iufumbue. Pia anasema kuwa vitendawili ni sanaa inayotegemea uwezo wa mtu kutambua, kuhusisha na kulinganisha vitu vya aina mbali mbali vilivyomo katika maumbile.

Misimu: ni semi za muda na mahali maalum ambazo huzuka na kutoweka kutegemea mazingira maalum, msimu ukipata mashiko ya kutosha katika jamii huweza kuingia katika kundi la methali za jamii hiyo.

Mafumbo: ni semi za maonyo au mawaidha ambazo maana zake za ndani zimefichika. Fumbo hubuniwa na msomaji kwa shabaha na hadhira maalum, hivyo ni tofauti na methali na vitendawili ambavyo ni semi za kimapokeo. Lakabu: ni majina ya kupanga ambayo baadhi ya watu hupewa au kujipatia kutokana na sifa zao za kimwili, kinasaba, kitabia au kimatendo. Majina haya huwa ni maneno au mafungu ya maneno yenye maana iliyofumbwa. Mfano: Sakarani inawakilisha Mlevi, Baba wa Taifa kwa Tanzania inawakilisha Mw.J.K Nyerere na Simba wa Yuda inawakilisha mfalme Haile Selassie.

TUKI (1990) wana maoni kwamba semi ni fungu la tungo za fasihi ambazo ni fupi fupi zenye kutumia picha, tamathali na ishara. Wanaendea kusema kuwa fungu la semi lina tanzu kama Misemo ambayo husemwa kuwa ni tungo zitumiazo picha,

ishara na tamathali kueleza kitu au wazo kwa ufupi, ili litolewe maadili au maonyo fulani. Katika kazi yao misemo inaonesha kuwa humithilisha maisha na matukio au vitu kwa mfano:

Mtoto wa nyoka ni nyoka.

Kuhusu mafumbo wameeleza kuwa utanzu huu una vijitanzu vya vitendawili na mizungu. Vitendawili ni semi fupi fupi za fumbo zenye kutumia picha, tamathali na ishara kueleza wazo lililofichika ambalo ndilo jawabu la fumbo. Mizungu ni vitendawili vinavyotumiwa katika miviga kueleza dhana na mawazo mbali mbali kwa maongezi au katika nyimbo. Mfano wa fumbo walilolitoa ni Miti yote nitakwea, mtarawanda unanishinda. Misimu wameisema kuwa ni semi ndogondogo za kupita ambazo huzushwa katika mazingira fulani na baadae kutoweka. Anasema kuwa aghlabu semi hizi ni za kitamathali. Mfano, Tamtam mahonda ukinila utakonda.

TUMI (1990) wana maoni yasemayo kwamba " semi ni fungu la tungo za fasihi ambazo ni fupifupi zenye kutumia picha, tamathali na ishara. Wameendelea kusema kuwa semi ina tanzu kama misemo waliyoifasili kuwa ni tungo zitumiazo picha ishara na tamathali kueleza kitu au wazo kwa ufupi. Wametoa mfano wa usemi usemao kwamba, *mtoto wa nyoka ni nyoka*. Katika mafumbo kuna utanzu wa vitendawili na mizungu.Uchunguzi wao unawiana na ule wa TUKI (1990).

Mbonde (2005) amefanya uchunguzi kuhusu methali za kiutandawazi, amesema kuwa lugha ya Kiswahili ni tajiri sana kwa semi zake. Licha ya methali kuna misemo, misimu na nahau. Katika uchunguzi wake amesema kuwa tofauti na

methali misemo ni tungo zitumiazo picha, ishara na tamathali kueleza kitu au wazo kwa kifupi ili litolewe maadili au maonyo au sifa fulani. Ameendelea kusema kuwa, vitendawili ni semi fupifupi za fumbo zenye kutumia picha tamathali na ishara kueleza wazo lililofichika ambalo ndilo jawabu la fumbo. Alitowa mfano wa wa fumbo lisemalo "*koti la mzee halikosi chawa"*.

Madumulla (2005) alieleza kuwa methali ni sentensi za ukweli zinazotokana na ujuzi, sharia na tabia za jamii ambazo kwa kawaida hushauri hatua za kuchukua au kupitisha maamuzi kuhusu jambo au kitendo fulani. Bukagile (2007) anaeleza kuwa semi ni tungo za fasihi simulizi ambazo ni fupi fupi zenye kutumia picha, tamathali za semi na ishara. Utafiti wake hautofautiani na watafiti wengine waliochunguza semi.

Mturo (2011) naye anaeleza kuwa semi ni kipengele cha fasihi simulizi ingawaje kwa sasa imo ndani ya fasihi andishi, hii ni kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia kwani inaweza kuhifadhiwa kwa maandishi. Kwa upande wa ugawaji wa semi yeye hakutofautiana sana na wataalamu wenzake akina Mulokozi (keshatajwa), ispokuwa yeye hakukigusia kipera cha lakabu. Naye Senkoro (2011) ameeleza kuwa semi kama misimu nahau na methali ni vipengele muhimu vya fani katika matumizi ya lugha. Jambo hii linatokana na ukweli kuwa vipengele hivi hutia mvuto katika kazi ya fasihi, na ameeleza kuwa methali zinatumika katika kuijenga fani na maudhui ya fasihi, kwani hutumiwa kama kutolea maadili na hata hekima kwa jamii husika. Kwa ujumla mawazo ya Senkoro mtafiti anayakubali kuwa semi ni kiungo muhimu cha kujengea kazi ya fasihi kwa kutumia kipengele cha lugha, na kwa maana hiyo mtafiti anasema kuwa mawazo haya yanatia mwanga katika utafiti wake huu,

mawazo ya kuwa, semi hupelekea kupatikana kwa hekima pamoja na busara katika jamii ni sahihi kwani utafiti huu umekusudia kugusia suala hilo. Mauya (2006) anaeleza kuwa semi ni fungu la maneno ambalo hupangwa kwa pamoja kisanii na kuleta maana isiyo ya kawaida. Kwa upande wa ugawaji wa semi yeye amezigawa sehemu tatu, nazo ni methali, nahau na misemo. Mtafiti wa utafiti huu hakubaliani kabisa na mgao alioutumia Mauya, kwani hakutaja mafumbo, vitendawili nawala misimu bali anasema tu kuwa semi nyingi ni mafumbo yenye kubeba ujumbe mzito.

2.2.2 Kazi Tangulizi kuhusu Semi

Semi zimefanyiwa utafiti na wataalamu wengi sana, miongoni mwao ni kama ifuatavyo:

Benard (keshatajwa) alifanya utafiti kuhusu ujitokezaji wa vipengele vya kimuundo, kidhamira na lugha katika misemo ya jamii ya Warombo kutoka Mkoa wa Kilimanjaro. Utafiti wake, pamoja na mambo mengine, ulibaini kwamba misemo ya jamii ya Warombo imejaa matumizi ya ishara, picha, taswira, mafumbo na sitiari. Kazi ya Benard (keshatajwa) imekuwa ni muhimu na ya msingi sana kwa utafiti huu kwa kuwa itachunguza jinsi tmathali za semi kama hizo lugha za ishara, picha, taswira, mafumbo na sitiari zinavyoweza kuibua maana za kimuktadha zilizokusudiwa kama itakavyobainiswa kwenye lengo la tatu la utafiti huu.

Mauya (2006) alifanya utafiti unaohusu maandishi katika vazi la kanga wanazovaa akina mama yeye alishughulikia migogoro pamoja na dukuduku ambazo akina mama huwa wanazo na zile wapendazo kufanyiana wao kwa wao. Migogoro hiyo na dukuduku hizo ni pamoja na masuala ya wivu, umbea wa wanawake, kufanyiana

fitina, kuchukuliana waume n.k. Haya yalielezwa kupitia misemo iliyoandikwa kwenye kanga. Kwa mtazamo huu basi mtafiti anaweza kusema kuwa anapata mwanga wa kufikia katika utafiti wake huu, kwani hayo yote ni masuala ya kiutamaduni, pamoja na mila na desturi ya watu wa Pemba. Anathubutu kusema kuwa binaadamu huweza kutumia semi kwa kuweza kufikisha yale ambayo yamekusudiwa. Pamoja na hayo Mauya uchunguzi wake haukuweka bayana baadhi ya mambo kama vile matumizi ya lugha. Utafiti wa Mauya umekuwa wa maslahi makubwa kabisa kwa kazi ya mtafiti wa kazi hii kwani mtafiti anafanya mada inayolingana kwa kiasi kikubwa, hivyo atapata ruwaza itakayomuongoza katika safari yake hii, ingawa mmoja Mauya anachambua fani na maudhui kifasihi, ilhali mtafiti wa kazi hii yeye anakusudia kuchambua vipengele vya kiisimu vinavyojitokeza katika semi za kanga.

Mahenge (2009) katika utafiti wake alichunguza semi katika tiketi zitumikazo kwenye daladala Mjini Dar es salaam, ambapo aligusia kipengele cha fani na maudhui. Kwenye uchunguzi wake huo aligundua kuwa baadhi ya semi zilikuwa ni methali na nyengine zilikuwa ni maneno tu ya kawaida, kupitia fani alichunguza tamathali za semi, picha, takriri, tash-hisi, sitiari, tash-biha na wahusika. Mtafiti huyu aligundua kuwa misemo iliyomo katika tiketi za daladala inaakisi maisha ya kila siku ya jamii, kupitia matumizi ya lugha na mitindo ya maandishi. Kupitia maudhui alichunguza dhamira zinazojitokeza katika tiketi hizo. Alibaini semi zilizomo humo zinaelezea umuhimu wa kufanya kazi, Kupiga vita ugonjwa wa UKIMWI, imani kwa Mungu, wajibu wa abiria, subira, ibada, ukarimu, mapenzi, ukweli, tabia njema na ushoga. Kwa ujumla utafiti wa maana Mahenge utausaidia utafiti huu wa

kuchunguza za kimuktadha katika semi zilizoandikwa katika kanga ingawa yeye alizungumzia fani na maudhui na sisi tutazungumzia maana za kimuktadha zilizomo humo. Ni ukweli kuwa yapo mambo ambayo yanafanana na hata kuwa na tofauti katika lugha na amegusia suala la maisha ispokuwa utafiti huu

Mturo (2011) alichunguza semi zilizoandikwa katika daladala na yeye alishughulikia kipengele cha matumizi ya lugha na dhamira.Katika utafiti wake yeye aligunduwa kuwa semi zilizoandikwa katika daladala zimetumia matumizi ya lugha kadhaa, kama vile tamathali za semi, methali na misemo. Kwenye dhamira zinazojitokeza katika daladala, hivyo hivyo zaweza kupatikana katika nyanja au kazi nyengine za fasihi kama vile ushairi, riwaya na hata tamthiliya. Ametoa mifano ya dhamira hizo kama ifuatavyo maadili, umuhimu wa kufanya kazi, imani kwa Mungu, na umoja. Kazi yake ina manufaa makubwa sana katika utafiti wetu huu. Hii ni kutokana na kuwa imeweka wazi matumizi ya lugha kwenye semi za daladala, ambapo na utafiti huu, unashughulikia semi zilizoandikwa katika kanga huku ukiangazia kipengele cha maana za muktadha zilizo ndani ya kanga zinazovaliwa kisiwani Pemba. Hata hivyo Mturo hakuzungumzia maana za kimuktadha zilizo kwenye semi zilizoandikwa kwenye kanga, kazungumzia semi za daladala tu. Hivyo utafiti huu umeweka bayana maana za kimuktadha zilizoandikwa kwenye kanga zinazovaliwa na jamii ya watu wanaoishi kisiwani Pemba.

Migodela (2011), kwa upande wake yeye alichunguza ufasihi wa misemo au semi zinazoandikwa katika sehemu za umma, alitoa mifano ya semi hizo zilizoandikwa katika kuta za vyooni. Matokeo ya utafiti wake huo inadhihirika kuwa semi zinazoandikwa kwenye kuta za vyoo zina matumizi ya lugha za kitamathali, mfano

tashbiha, sitiari, ishara, taswira, (tafsida) badala yake zinaeleza mambo wazi wazi bila ya kuficha kitu. Utafiti wa Migodela (keshatajwa) unachangia kwa kiasi kikubwa katika utafiti huu kwa kutoa mwanga juu ya tafsida, picha n.k. Kwa kuongezea aligunduwa kuwa semi nyengine hazitumii lugha ya kuficha matumizi ya lugha aliyoyatumia katika semi za chooni. Kwa muktadha huo, utafiti wetu huu unatumia mbinu hizo hizo kama vile sitiari, ishara n.k. katika semi zilizoandikwa katika kanga zinazovaliwa na jamii ya wanawake wanaoishi Pemba. Tofauti iliyopo katika utafiti wa Migodela na utafiti huu ni kuwa sisi tunachunguza kipengele maana ya kimuktadha zinazojitokeza katika kanga zinazovaliwa na wanawake wa jamii ya Wapemba ilhali yeye kazungumzia katika semi zilizoandikwa katika kuta za chooni.

Alhabib (2012) alifanya uchunguzi unaohusiana na matumizi ya taswira katika nyimbo za taarabu, na matokeo ya utafiti wake huo aligundua kuwa kipengele cha misemo kinajidhihirisha katika nyimbo za taarabu. Ni nadra kuisikia nyimbo ya taarabu isiyokuwa na misemo japo kidogo. Ndani ya semi hizo ndimo munamopatikana ufikishaji wa dhamira mbalimbali kwa wasikilizaji wake. Utafiti huu wa Alhabib kama alivyoona mtafiti una mchango mkubwa sana katika kufanikisha utafiti wake, kwani umebainisha kuwa semi zinaweza kujitokeza katika nyanja nyengine na kupelekea kupatikana makusudio ya mtunzi wa kazi fulani ya fasihi. Tunahitimisha kwa kusema kuwa utafiti wetu huu umekuwa imara kwa kugusia nyanja ambazo Alhabib hakuzieleza katika utafiti wake, kwa mfano yeye hakuzungumzia maana za kimuktadha zilizo katika semi zilizoandikwa, katika kanga zinazovaliwa na wanawake wa jamii ya Wapemba ambapo zimewekwa bayana

katika utafiti huu na zinakuwa zinaonesha hali halisi ya maisha ya Wapemba. Yeye aligusia matumizi ya taswira katika nyimbo za taarabu.

Naye Uled (2012) alichunguza muundo na vipengele vya lugha katika methali na vitendawili kwa jamii ya Wamakunduchi, kwa kulinganisha semi hizo na zile za Kiswahili rasmi. Katika uchunguzi wake aligunduwa kuwa katika methali na vitendawili kuna vipengele mbalimbali vya lugha vinavyotumika katika ujenzi wake. Uchunguzi wake una mchango mkubwa katika kufanikisha utafiti huu kwani utafiti huu nao unachunguza semi na umekusudia kuchunguza kipengele cha maana za kimuktadha zilizo katika semi zilizoandikwa katika kanga zinazovaliwa na kinamama wa jamii ya Wapemba.

Naye Rajabu (2012) alichunguza dhima ya misemo iliyoandikwa katika fulana, kwa kushughulikia kipengele cha dhamira na matumizi ya lugha katika jiji la Dar es Salaam. Matokeo ya utafiti wake aligunduwa kuwa vazi la fulana limesheheni dhamira mbalimbali, alizitaja dhamira hizo kuwa ni; UKIMWI, dini, umasikini, hali ngumu ya maisha, wivu na chuki, maisha, elimu, umuhimu wa kufanya kazi na pesa. Ametambulisha kwamba dhamira zimekubaliana na mambo yaliyopo katika jamii. Katika kipengele cha lugha amegundua kuwa maandishi yaliyomo kwenye fulana yana matumizi ya lugha, vipengele alivyovitaja ni pamoja na tamathali za semi, majigambo, misemo na maneno ya mitaani. Utafiti wa Rajabu una mchango mkubwa katika utafiti huu kwenye kipengele cha matumizi ya lugha. Hata hivyo kuna baadhi ya tofauti zinazojitokeza ambazo ni: Kwanza, Rajabu kachunguza semi kwenye fulana zinazovaliwa jijini Dar es salaam na utafiti huu unachunguza semi zilizoandikwa katika kanga kwa kuangalia maana za kimuktadha zilizojitokeza.

Na hatimaye tumuangalie Hassan (2013) ambaye alifanya utafiti kuhusu dhima ya methali katika jamii ya Wapemba. Katika uchunguzi wake amebaini kuwa methali zinatumika katika jamii ya Wapemba kwa kuangalia dhima ili kudumisha dhamira na maadili katika jamii na matumizi ya methali katika jamii kwa ujumla katika miktadha mbalimbali. Miktadha iliyozingatiwa ni pamoja na muktadha wa Pwani, muktadha wa shuleni, muktadha wa sokoni, muktadha wa Dini, muktadha wa shughuli za kazi, muktadha wa shughuli za kisiasa nakadhalika. Uchunguzi wake una manufaa makubwa kwa utafiti huu kwani kachunguza dhima ya methali katika kudumisha dhamira na maadili katika jamii ya Wapemba, ambapo mtafiti wa utafiti huu naye anachunguza dhima za semi, lakini katika kuangalia maana za kimuktadha zilizojitokeza katika kanga zinazovaliwa na kinamama wa jamii ya Wapemba. Hivyo basi, uchunguzi wa Hassan (keshatajwa) umetoa dira ya kufanikisha utafiti huu kufikia malengo yake kwa kuziba pengo lililoachwa la kueleza dhima za semi zilizoandikwa katika kanga.

2.3 Kiunzi cha Nadharia

Kazi yoyote ile ya utafiti ni lazima itumie nadharia ambayo inakubaliana au kushabihiana na kazi hiyo.

2.4 Maana ya Nadharia

Massamba (2004:63) anasema kwamba nadharia ni kanuni na misingi ambayo hujengwa katika muundo wa kimawazo kwa madhumuni ya kutumiwa kama kielelezo cha kueleza jambo. Kwa mujibu wa fasili hiyo neno nadharia linamaanisha maelezo ya jambo yaliyofungamana na vigezo vilivyowekwa au vilivyozalishwa kutokana na uchunguzi yakinifu uliofanywa na kuthibitika kwa ushahidi wa

kisayansi. Vigezo hivyo ndivyo vinavyounda kanuni na msingi wa kulieleza jambo lililokusudiwa. “Nadhria ni mawazo maelezo au muongozo uliopangwa ili kusaidia kueleza, kutatua au kutekeleza jambo fulani” (Kamusi la Kiswahili Sanifu 2004:200). Kamusi kamili ya Kiswahili (2009:363) inaelaza kuwa nadharia ni “mpango wa mawazo au muongozo uliotungwa ili kueleza jinsi ya kufanya au kutekelaza jambo fulani”. Mushengezi (2003) naye anasema kuwa nadharia ni maarifa yaliyopangwa ili kueleza dhamira fulani au wazo fulani. Nadharia huchukuliwa kuwa ni dira ya kumuongoza mtafiti au mchambuzi kulikabali na kulielezea vyema jambo fulani kwa mtazamo ambao mtafiti ameujengea imani kwamba unaweza kuleta manufaa zaidi kuliko mtazamo mwengine pindi ukitumika. Nadharia hutoa muongozo katika kutatua jambo ambalo halijaweza kuhakikishwa ukweli wake.

Hivyo basi kwa mada hii ya “Kuchunguza maana za kimuktadha katika kanga zinazovaliwa na kina mama kisiwani Pemba. Mtafiti ametumia nadharia ya maana ya Ludwing Wittgenstein (1953) . Katika kazi hii alitumia nadharia mbili ambazo ni (i) Nadharia ya Maaana ya Matumizi (ii) Nadharia ya Maana ya Kimuktadha

2.4.1 Nadharia ya Maana ya Matumizi

Muasisi wa nadharia hii ni Ludwing Wittgenstein (1953) na imeelzwa katika kitabu cha Philosophical Investigetion (Riemer 2010, Akmajian na wenzake 2010). Wittegnstein (keshatajwa) anaeleza kuwa ni kosa kubwa kuweka mipaka ya maana kama ambavyo nadharia ya maana kama dhana, mwitiko na kitajwa zinavyofanya, kwani kufanya hivyo ni sawa na kuweka mipaka ya thamani ya umbo lenyewe la kiisimu. Kinachopaswa kuzingatiwa ni matumizi ya nadharia, nadharia hii inajikita

na kusisitiza kuwa maana ya neno katika lugha ni matumizi yake. Hivyo haina haja ya kuuliza neno hili lina maana gani bali angalia vipi neno hilo linavyotumika. Ullman (1967), Lyons (1987); Fodor (1980), Akmajian na wenzake (2010) pamoja na Reimer (2010) kwa upande mwengine wanaeleza kuwa namna bora ya kueleza maana kisayansi ni kuepuka dhana zisizoonekana wala kuthibitika na badala yake tuangalie uhalisiya, yaani matumizi ya lugha kwa kuzingatia muktadha. Wittgenstein (keshatajwa) anafafanua zaidi kuwa lugha hufungamanishwa na tabia zetu na namna tunavyohusiana na watu wengine. Tunatumia lugha kutoa amri, kujibu maswali, kusalimiana na kadhalika. Hivyo lugha lazima itazamwe kama kifaa na sio kitu dhahania. Uelewaji wa maana ya umbo lolote lile la kiisimu ni lazima uzingatie namna lugha inavyotumika. Katika kushadidia zaidi juu ya umuhimu wa nadharia hii, Tobing (2010) anaeleza kuwa maana za maneno hazitakuwa na uvulivuli kama zitakitwa katika muktadha matumizi. Akitililia mkazo zaidi juu ya umuhimu wa nadharia hii Fodor (1980) anaeleza kuwa nadharia hii haibagui umbo lolote la kiisimu lenye maana. Maneno ya Kiswahili kama vile kwa, na, ya, wa hayana kitajwa wala kuashiria dhana fulani akilini, lakini huweza kuelezwa kwa kutumia nadharia hii ya maana kama matumizi. Wijaya na Yeniterzi (2011) wanaeleza kuwa maneno hubadilika kimaana na mabadiliko hayo huakisiwa katika namna au jinsi maneno hayo yanavyotumika katika miktadha tofauti. Kasoro ya nadharia hii ni kwamba kuelewa maana hakuleti uelewa wowote wa neno hadi liwe katika matumizi. Kwa mfano neno “mbuzi “linapata maana kulingana na linapotumika kama ni kifaa cha kukunia nazi au ni aina ya mnyama. Akmajian na wenzake (2010) wameainisha udhaifu wa nadharia hii kuwa haijaweka wazi mipaka ya kimatumizi ni ipi. Pamoja na mapungufu hayo kuteuwa kwa nadharia hii sio kwa kiholela tu bali

kwa kuzingatia ubora wake hasa katika kuelezea maana ya semi zilizoandikwa katika kanga zinazovaliwa na kina mama kisiwani Pemba. Maana za kimuktadha hazitolewi kwa kuangalia umbo la neno katika mazingira ya kawaida.

2.4.2 Nadharia ya Maana Kimuktadha

Waasisi wa nadharia hii ni Wanaisimu ambao wanadai kuwa maana ya neno, dhana au hali fulani hutokana na muktadha uliopo au unaowazunguka watumiji wa lugha. Katika nadharia hii muktadha hupewa nafasi muhimu katika ufasiri wa maana. Nadharia hii hupinga matumizi ya kamusi katika kufafanua maana kwa msingi kwamba kamusi haibainishi muktadha wa matumizi ya neno husika. Wanaisimu hawa waliainisha aina tatu za muktadha. Muktadha wa kijamii, muktadha wa usemi na muktadha wa kiisimu. Kwa kuzingatia muktadha wa kijamii kuna baadhi ya maneno ambayo huwa na maana katika jamii fulani na yasiwe na maana katika jamii nyingine. Vilevile yapo baadhi ya maneno ambayo yana maana katika mazingira fulani kimuktadha lakini kayana maana katika mazingira hayohayo katika hali ya kawaida. Muktadha wa usemi huongoza uteuzi wa matumizi ya maneno mbalimbali. Hivyo matumizi ya kila neno lazima yaendane na muktadha mwafaka. Kwa mfano “chai moja” usemi huu huendana na muktadha wa hotelini. Usemi huu ukitumiwa kwenye nyumba za ibada utazua utata. Sungura alipokuwa porini akaona matunda mtini yameiva, alipoyarukia akashindwa kuyakamata, alisema “sizitaki mbichi hizi” kumbe ni muktadha tu ulimlazimisha kusema hazitaki mbichi hizo, lakini ukweli unabakia pale pale kwamba sungura alitamani sana zile ndizi juu ya mti (Mnata 2014). Nadhria hii imemsaidia mtafiti wa kazi hii hasa katika kubainisha maana za kimuktadha katika semi zilizoandikwa kwenye kanga zinazovaliwa na kina mama

kisiwani Pemba kama ilivyobainishwa kwenye lengo la pili. Kutokana na namna ya matumizi ya semi hizo ambazo zaidi zinatafsiriwa kimuktadha.

Nadharia ya Simiotiki

Kimambo (2015) anaeleza kwamba; Simiotiki ni nadharia inayohusika na uchambuzi wa masuali ya lugha inayotokana na nadharia ya Umuundo iliyoasisiwa na Fednarnd De Saussure mwaka 1966. Nadharia hii kwa ujumla inazungumzia namna lugha inavyotumika kama chombo cha kiishara chenye kuwezesha mawasiliano baina ya watu katika jamii. Saussure anaeleza kuwa katika lugha huwa kuna vitu viwili ambavyo ni kitaja na kitajwa. Kitaja ni jina linalotaja kitu fulani na kitajwa ndio kile kinachorejelewa na jina hilo. Mtaalamu huyu anaendelea kueleza kuwa katika hali ya kawaida, hakuna uhusiano wa moja kwa moja baina ya kitaja na kitajwa, bali uhusiano uliopo ni wa kubuni tu.

Othmani (2018) akimrejelea Brown (1995) anasema ishara hupata maana kutokana na matumizi yake. Ili watu waelewe kinachowasilishwa na ishara fulani, lazima watu hawa wawe na makubaliano fulani ambayo hutokana na kushiriki elimu, utamaduni, dini na mandhari sawa. Ishara hizi hujumuisha picha, rangi, maumbo mbalimbali, na hata herufi zinazounda maneno. Watu wenye asili moja huweza kuelewa ishara sawa kwa njia tofauti ikitegemea utamaduni, lugha na makubaliano kuhusu ishara fulani na maana zake. Ferdnand de Saussure (1857-1913), Charles Pierce (1839-1914) na Rolland Barthes (1915-1980) ni miongoni mwa waasisi wa nadharia ya Simiotiki, wanaeleza kuwa Simiotiki kama kanuni za ishara zinazowakilisha mtu au kitu katika hali fulani. Nadharia hii ina misingi

yake katika imani kuwa watu katika jamii moja wanaozungumza lugha moja na kuwa na utamaduni sawa huweza kuwasiliana kwa njia fiche.

Wamitila (2002) anaeleza kuwa Simiotiki ni nadharia inayohusika na uchunguzi wa lugha ya picha, ishara, mafumbo na taswira katika kazi ya fasihi. Watunzi wa kazi za fasihi hutumia lugha ambayo si ya kawaida kuelezea matukio ya kwaida katika jamii ili kusawiri hali halisi ya maisha. Matumizi ya lugha ya kiishara na uashiriaji katika kazi za fasihi, hujitokeza katika misimbo ya aina tano inayotajwa na Barthes (1994). Misimbo hiyo ni msimbo wa kimatukio, msimbo wa kihemenitiki, msimbo wa kiishara, msimbo wa kiseme na kitamaduni (kiurejelezi). Misimbo hii imetolewa ufafanuzi kama ifuatavyo:

Msimbo wa matukio: Msimbo huu unahusu namna matukio yanavyopatikana katika hadithi, yanavyofutana na jinsi msomaji anavyounda na kuelewa msuko wa kazi ya fasihi.

Msimbo wa Kihemenetiki: msimbo huu unahusu taharuki na usimulizi. Msimbo huu kwa jina jengine huitwa msimbo wa kusimulia au msimbo wa kutamba hadithi na unaweza kufumbatwa kwenye anuani ya kazi.

Msimbo wa Kiishara: msimbo huu wa kiishara unahusishwa na namna wasomaji wanavyofumbua maana za ishara katika kazi za fasihi.

Msimbo wa Ki-seme: Msimbo huu hueleza elementi nasibishi za kisemantiki ambapo hutupatia picha ya muhusika fulani wa kifasihi.

Katika kuzisoma na kuzihakiki kazi mbalimbali za kifasihi, matumizi ya lugha hujidhihirisha katika misimbo mitano iliyotajwa. Mtumizi hayo ya lugha hubainika na kuweza kutoa taswira ya dhamira zilizokusudiwa na mwandishi na kuweza kupata undani wa kazi ya kifasihi kama ilivyokusudiwa na mwandishi.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Sehemu hii itafafanua mpango mzima wa utafiti, na jinsi utafiti huo utakavyofanywa:-

Vipengele vitakavyochambuliwa kwenye eneo hili ni pamoja na eneo la utafiti, mbinu zitakazotumika kukusanyia data za utafiti, muundo wa utafiti, usampulishaji, zana zitakazotumika katika utafiti.

3.2 Eneo la Utafiti

Lengo la utafiti huu lilikuwa ni kubainisha semi mbali mbali zilizoandikwa katika majina ya kanga na kuchambua maana za kimsamiati na za kimuktadha zilizoandikwa katika kanga zinazovaliwa na watu wa Pemba, kama ilivyokwishaelezwa hapo mwanzo. Ingawa vazi la kanga linavaliwa takriban katika eneo kubwa la ukanda wa Afrika Mashariki na nchi jirani, katika utafiti huu tuliamua kuufanya katika kisiwa cha Pemba kwenye shehia za Kiwani, Kinyasini, Makombeni wilaya ya Mkoani Mkoa wa Kusini Pemba.

Mtafiti amechagua kisiwa cha Pemba kutokana na mtafiti kuyaelewa vizuri maeneo husika, jambo ambalo lilipelekea urahisi wa kukusanya data.Vile vile katika kisiwa cha Pemba ndiko tulikoweza kupata maana za majina ya kanga kiurahisi kwa vile mtafiti anaishi na ni mwenyeji wa Pemba. Pia Wapemba ndio walioweza kuzitolea ufafanuzi maana hizo, isitoshe wao walikuwa ni mahiri katika kujua maana za

kimsamiati na maaana za kimuktadha zilizojitokeza katika majina ya kanga kwa vile kanga ndio vazi kuu kisiwani Pemba.

Jambo jingine la msingi katika kuchagua eneo hili ni kwamba katika kupitia maandiko mbalimbali hatukugundua maandishi yoyote yaliyozungumzia maana za majina ya kanga zinazovaliwa na watu wa Pemba, hivyo tuliona ni vyema kulichagua eneo hili ili kutekeleza malengo ya utafiti.

3.2.1 Usampulishaji

Best (1996) anasema kwamba, usampulishaji ni njia au utaratibu wa kuteua washiriki wachache kutoka katika kundi kubwa la jumla la watafitiwa wote. Mtafiti wa utafiti huu atateua miongoni mwa wazee, baadhi ya vijana na watu wa makamo wenye uwelewa juu ya semi zilizojitokeza katika majina ya kanga ili kuwawakilisha watafitiwa wengine katika jamii lengwa iliyoteuliwa.

3.2.2 Sampuli

Babbie (1999:205) ameifasili sampuli kuwa ni kundi dogo la watafitiwa ambalo wamechaguliwa katika kundi kubwa kwa lengo la kutoa data za kuwakilisha kundi zima. Sampuli iliyolengwa katika kutoa taarifa za utafiti huu ilijumuisha rika ya wazee, watu wa makamo na vijana. Vijana thelathini na tano (35), wanawake ishirini (20) na wanaume kumi (15) sawa na asilimia 32% ya sampuli wote. Wazee waliohojiwa ni thelathini (45) wanaume kumi (20), wanawake ishirini (25) sawa na asilimia 41% ya sampuli wote. na watu wa makamo (30) wanaume kumi (16) na wanawake kumi (14) sawa na asilimia 27% ya sampli wote . Jumla yao ni 110. Mchanganuo huu umewasilishwa kwa muhtasari katika jedwali lifuatalo:

Jedwali na 1 : Idadi ya Sampuli

KUNDI	UMRI	WANAWAKE	WANAUME	JUMLA	ASILIMIA
Vijana	18-39	20	15	35	32%
Watu wa makamo	40-59	14	16	30	27%
Wazee	60-70	25	20	45	41%
JUMLA		**59**	**51**	**110**	**100%**

3.3 Mkabala wa Uchambuzi wa Data

Mbinu mbalimbali zilizotumika katika utafiti huu ili kuweza kufanikisha kazi hii. Mtafiti aliwahoji watafitiwa kwa kutumia njia ya mahojiano ya ana kwaana na njia ya uchunguzi makini ambazo katika mazingira tofauti ambapo semi zilizoandikwa katika majina ya kanga zimepatikana na kutoa maana ya muktadha. Mtafiti amechambua data baada ya kurudi kuhoji na kukusanya data kwa mbinu ya maelezo na kimahesabu . Katika kuchambua maana za kimuktdha mtafiti alitumia nadharia maana ya kimuktadha na nadharia ya maana ya kimatumizi. Katika majina ya kanga, utafiti umetumia mbinu ya ufafanuzi, mbinu ambayo ni ya kutumia maelezo na kimahesabu katika kuchanganua data. Data zimekusanywa, mtafiti amejaribu kadri awezavyo na kuziweka pahali pamoja ili zilingane na yale malengo yake ya utafiti. Vile vile kuangalia uhusiano wa data hizo alizozikusanya. Kila lengo moja la utafiti huu, wazo ambalo jedwali mbalimbali na amezitafsiri data zake kwa kutumia michoro ya kitakwimu zilizosaidia kuwa ni mada ndogondogo za utafiti zilizojumuishwapamoja. Licha ya maelezo mtafiti atatumia mia data zake kutoa ulinganifu wa data zilizo kusanywa.

3.4 Njia za Ukusanyaji wa Data

Kothari (2008) anasema kwamba mbinu za utafiti ni muhimu sana katika kufanya uchunguzi wa kitaaluma. Kutokana na mbinu hizo ndipo utafiti unaweza kufanyika kisayansi. Walliman (2005) anaeleza kuwa ziko mbinu mbili ambazo mtafiti anaweza kuzitumia kwa kukusanyia data, mbinu za kukusanya data uwandani na mbinu za kukusanya data maktabani. Katika utafiti huu mtafiti atatumia mbinu changamano yaani mbinu ya uwandani na mbinu ya maktabani.

3.4.1 Mahojiano (Usaili)

Kombo (2006), Mahojiano ni majibizano ya ana kwa ana au uso kwa uso, kwa mawasiliano ya simu, barua pepe nakadhalika yanayofanywa na watu wawili au zaidi kwa lengo la kukusanya data. Mtafiti wa utafiti huu alitumia mahijiano ya ana kwa ana na watafitiwa wake. Sababu ilyomfanya mtafiti kutumia njia hii ni kuwa katika mahojiano mtafitiwa anakuwa yuko huru kwa kutoa data zenye usahihi, na ni njia inayompa fursa ya kuuliza maswali pale panapohitajika.

3.4.2 Uchunguzi Makini

Uchunguzi ni mbinu ya kukusanya data inayohusiana na kurikodi tabia za watu, vitu na matukio katika mpangilio maalumu. Hii ni njia ambayo inafanyika kwa kukusanya data inahusika na kurikodi watu, matukio mbalimbali na hata vitu kwa mpangilio maalum Walliman (2005)

(keshatajwa) kuwa data za awali ni data zinazoaminika kwasababu hupatikana au kurekodiwa moja kwa moja kutoka kwenye tukio.

3.5 Mkabala wa Uchambuzi wa Data

Mbinu mbalimbali zilizotumika katika utafiti huu ili kuweza kufanikisha kazi hii. Mtafiti aliwahoji watafitiwa kwa kutumia njia ya mahojiano ya ana kwaana na njia ya uchunguzi makini ambazo katika mazingira tofauti ambapo semi zilizoandikwa katika majina ya kanga zimepatikana na kutoa maana ya muktadha. Mtafiti amechambua data baada ya kurudi kuhoji na kukusanya data kwa mbinu ya maelezo na kimahesabu . Katika kuchambua maana za kimuktdha mtafiti alitumia nadharia maana ya kimuktadha na nadharia ya maana ya kimatumizi. Katika majina ya kanga, utafiti umetumia mbinu ya ufafanuzi, mbinu ambayo ni ya kutumia maelezo na kimahesabu katika kuchanganua data. Data zimekusanywa, mtafiti amejaribu kadri awezavyo na kuziweka pahali pamoja ili zilingane na yale malengo yake ya utafiti. Vile vile kuangalia uhusiano wa data hizo alizozikusanya. Kila lengo moja la utafiti huu, wazo ambalo jedwali mbalimbali na amezitafsiri data zake kwa kutumia michoro ya kitakwimu zilizosaidia kuwa ni mada ndogondogo za utafiti zilizojumuishwa pamoja. Licha ya maelezo mtafiti atatumia data zake kutoa ulinganifu wa data ziliz kusanywa.

3.6 Hitimisho

Sura hii imejadili na kuelezea kwa kina mbinu na njia mbalimbal zilizotumika katika kufanikisha kazi hii. Sura imejumuisha eneo la utafiti, muundo wa utafiti, uteuzi wa watafitiwa, usampulishaji, sampuli, mkabala wa uchambuzi wa data.

SURA YA NNE

UCHAMBUZI NA UWASILISHAJI WA DATA

4.1 Utangulizi

Katika sura hii mtafiti alichambua data mbalimbali, ambazo zimekusanywa moja kwa moja kutoka katika vianzio mbalimbali vya data kama vilivyoelezewa katika sura ya chambuzi na uwasilishaji wa data umefanywa ili kubainisha kuwa yale malengo ya utafiti huu yamefikiwa kama ilivyotarajiwa na mtafiti .

Sura hii inatambulisha semi zinazotumiwa na watu wa Pemba hasa katika semi zilizotumika katika majina ya kanga zinazovaliwa na kina mama wa kisiwa cha Pemba.

4.2 Utafiti na Malengo yake

Katika utafiti huu kulikuwa na nadharia ya maana ya matumizi na nadharia ya maana ya muktadha ambayo ilitumika kwa kuchambua maana za kimsamiati na maaana za kimuktadha zilizoandikwa katika majina ya kanga. Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza maana za muktadha zilizojitokeza katika semi zilizotumika katika majina ya kanga zinazovaliwa na kina mama wa kisiwa cha Pemba . Na malengo mahsusi yalikuwa ni kama ifuatavyo:-

i. Kubainisha semi mbali mbali zilizoandikwa katika kanga.

ii. Kubainisha maana za kimsamiati za semi teule zilizoandikwa kwenye kanga.

iii. Kuchambua maana za muktadha za semi teule zilizoandikwa kwenye kanga.

4.2.1 Kubainisha Semi Mbali mbali zilizoandikwa katika Kanga

Suala hili liljibiwa na jumla ya watafitiwa 110 sawa na asilimia 100%. Wanawake waliojibu swali hili ni hamsini na tisa (59). Watafitiwa ishirini (20) wanawake vijana sawa na asilimia 34% ya wanawake wote waliohojiwa, Watafitiwa kumi na nne(14) wanawake wa makamo sawa na asilimia 24% ya wanawake wote waliohojiwa na wanawake 25 sawa na asilimia 42% ya wanawake wote walijibu kwamba wanazifahamu semi zilizoandikwa katika kanga. Kwa upande wa wanaume watafitiwa hamsini na moja walihojiwa na kutowa jibu la kutambua kuwepo kwa semi zilizoandikwa katika kanga.Vijana walikuwa ni kumi na tano(15) sawa na asilimia 29% , wanaume wa makamo walikuwa ni kumi na sita(16) sawana asilimia 31% na wazee watu wazima walikuwa ishirini (20) sawa na asilimia 40%. Wote hawa kwa ujumla walijibu kuwa nidyo wanazifahamu semi zilizoandikwa katika kanga., Kuhusu suala hili hakuna mtafitiwa aliyejibu hapana. Kwa mantiki hiyo inaonesha kwamba watu wengi wanazijuwa semi zilizoandikwa katika kanga.

Mtafiti baada ya kuchambua data zinazohusiana na semi zilizoorodheshwa na watafitiwa, alichagua semi 109 kati ya semi 159 zilizotajwa na watu wa makamo, wazee na vijana. Katika sehemu hii mtafiti amezigawa semi hizo katika makundi mbalimbali,. Zipo semi ambazo zinahusu mila na utamaduni wa jamii, dini na imani, bidii katika kazi, elimu, na subira pamoja na uvumilivu.

Semi zinazohusu mila na desturi za jamii ni 30, semi zinazohusu dini na Imani 26, semi zinazoelezea bidii na kazi 14, semi zinazohusu elimu 19, semi zinazohusu subira na uvumilivu 15 na semi zinazohusu ushirikiano 5. Semi hizo zinaonekana katika orodha mbalimbali kama ifuatavyo:

4.2.1.1 Semi zilizoandikwa katika Kanga zenye kuhusu Mila na Utamaduni wa Jamii

1. Japo sipendezi kubembeleza siwezi.
2. Usione nimetulia mengi nimevumilia.
3. Cheka nao uwajue tabia zao.
4. Chunga chungio usinichunge mie si mke mwenzio.
5. Samaki akioza usimtupe watu watakujamuokota uje ujute
6. Bora kujikwaa dole kuliko ulimi
7. Masikini naye mtu japo kuwa hana kitu.
8. Tulia tuishi wazuri haweshi.
9. Hata ukinisukuma wa mbele harudi nyuma
10. Mcheza kwao hutunzwa
11. Sitokula gizani kwa kumuogopa jirani
12. Nna roho sina jiwe mengine nipunguziwe
13. Usigeuke kuku kupekua huku na huku
14. Baniani mbaya kiatu chake dawa
15. Mbaya halisi na wema hakosi
16. Bora umasikini wangu kuliko utajiri wa mwenzangu
17. Namuogopa simba kwa meno yake simuogopi mtu kwa maneno yake
18. Usimlaumu paka wangu chungu chako umekiacha wazi
19. Mzizi sio jadi yangu kupendwa ni bahati yangu
20. Mpewa hapokonyeki
21. Ukipenda boga upende na mti wake
22. Machoni rafiki rohoni mnafiki

23. Nasema na bwana mkaa kitini sisemi na kuku mchakura chini
24. Usipende uadui ataekufaa humjui
25. Tutabanana hapahapa
26. Kanipenda mimi binafsi kama una donge kalilie polisi
27. Kama mimi mbaya mwema nani
28. Nenda wendako ukirudi mimi wako
29. Waona ya wenzao wasahau yao
30. Unapita mpakani kwangu halahala na mbaazi zangu

4.2.1.2 Semi zilizoandikwa katika Kanga zenye Uhusiano wa Dini na Imani

1. Mpaji ni Mungu.
2. Dunia isituhadae turudi kwa Mungu
3. Mola tupe kheri tupate yalo mazuri
4. Nia njema hairogwi
5. Kazi ya Mungu haina makossa
6. Riziki haiwanywa
7. Unawashukuru watu unamkufuru Mungu
8. Ewe Mola wangu ibariki ndoa yangu
9. Mke mwema hutoka kwa Mungu
10. Jipe moyo utashinda
11. Nyumba ya maskini haishi kujengwa

12. Machozi ya mnyonge malipo kwa Mungu

13. Kwa yote uliyonifanyia Mola atanilipia

14. Alokamilika Mungu safi kiumbe hakuna

15. Mungu ni muenza wa yote

4.2.1.3 Semi zilizoandikwa katika Kanga zinazohusu Maarifa Mengineyo

1. Kikulacho kinguoni mwako

2. Kaza roho umeze fupa

3. Lima juani ulie kivulini

4. Hala hala ujiti na macho

5. Ukupigao ndio ukufunzao

6. Bora kujikwaa dole kuliko ulimi

7. Mtaka cha mvunguni sharti ainame chini

8. Ndege mjanja hunasa tundu bovu

9. Kama ni wewe waweza

10. Mke hapigwi kwa fimbo

4.2.1.4 Semi zilizoandikwa katika kanga zinazohusu Bidii katika Kazi

1. Hamadi kibindoni silaha mkononi
2. Jembe halimtupi mtu

3. Lima juani ulie kivulini

4. Penye nia ipo njia

5. Mcheza kwao hutunzwa

6. Mtarazaki hachoki

7. Mtu ni chake

8. Mti hawendi ila kwa nyenzo

9.Ukijitahidi utafanikiwa

10. Bandu bandu huishia gogo

4.2.1.5 Semi Zinazohusu Subira na Uvumilivu

1.Awali si hoja bora hatima

2. Kaza roho umeze fupa

3. Subira ni ufunguo wa peponi

4.Mpewa hapokonyeki

5. Mwenda pole hajikwai

6. Mstahamilivu hula mbivu

7. Nimeonesha busara mbona sasa mwanikera

8. Nayapuuza ndio maana siyumbi

9. Kofi la mama nalia la mpenzi navumilia

10. Sitolipiza wala sitosahau

4.2.1.6 Semi Zilizoandikwa katika Kangazinazohusu Ushirikiano

1. Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu
2. Wingi wa mchanga ni mchanga wa funguni
3. Tuwa tugawe
4. Wengi wape
5. Nguvu ya maji ni mawe

4.2.2 Uainishaji wa Maana za Kimsamiati na Muktadha wa Semi Teule

Lengo la pili mahsusi katika utafiti huu lilikua ni kutoa maaana ya kimsamiati na muktadha katika semi zilizoandikwa kwenye kanga kwa mujibu wa data zilizokusanywa:

4.2.2.1 Semi zilizoandikwa kwenye kanga zenye kuhusu Mila na Utamaduni wa Jamii

Katika eneo hili mtafiti ameteua semi kumi na mbili na kueleza maana zake za kimsaniati na muktadha kama ilivyo kwenye jedwali na 1. Hapo chini:-

Jedwali na. 2: Semi zilizoandikwa kwenye kanga zenye kuhusu Mila na Utamaduni wa Jamii

Na	Semi	Maana zakimsamiati	Maana za kimuktadha
1	Bora kujikwaa dole kuliko ulimi	Bora kujikwaa katika sehemu ya mguu kuliko kujitafuna ulimi	Bora kufanya kusa jengine lolote kuliko kuutumia mdomo vibaya
2	Samaki akioza usimtupe watu watakujamuokota uje utute	Samaki anapoharibika umtengeneze tengeneze tu huenda akalika	Mke anapokuwa na tabia ambazo sizo umulekeze huenda akaelewa ujapoukamuacha anaweza kupata mtu akamuelekeza akaelewa ukajajuta
3	Mcheza kwao hutunzwa	Mtu anapocheza kwao inapendeza atunzwe	Mtu anafanya jambo zuri apewe motisha chanya
5	Tutabanana hapahapa	Kubanana katika sehemu moja kwa kukaa karibu na mtu mwengine	Maisha ya kiukewenza dhidi ya mume
7	Unapita mpakani kwangu hala hala na mbaazi zangu	Unapita pembezoni mwa shamba langu jihadhari na matunda yangu	Unajikaribisha nyumbani nakuhadharisha na mke wangu
10	Kanipenda mimi binafsi kama una donge kalilie polisi	Kupendwa ni bahati ya mtu hata ukashitaki kwenye chombo cha sharia	Mapenzi hayalazimishwi na mashitaka hayana nafasi
11	Usimlaumu paka wangu chungu chako umekiacha wazi	Unapokiwacha chungu chako wazi inaonesha wazi kuwa kitoweo chako paka atakila	Unaposhindwa kufata maadili yanayotakikana na ukaenda kombo basi watu watakudhuru
12	Usipende uadui ataekufaa humjui	Usipende ushari atakae kufariji humjui	Usishadidie uovu mwema wako humtambui

Chanzo cha Data: Uwandani

4.2.2.2 Semi Teule zilizoandikwa kwenye Vazi la Kanga zenye Uhusiano wa Dini na Imani

Katika eneo hili mtafiti ameteua semi kumi na mbili na kueleza maana zake za kimsaniati na muktadha kama ilivyo kwenye jedwali na 2 hapo chini:

Jedwali na. 3: Semi zilizoandikwa kwenye kanga zenye kuhusu Dini na Imani

Na	Semi	Maana zakimsamiati	Maana za kimuktadha
1.	Mpaji ni Mungu.	Mtoaji ni Mungu	Mung undie mtoaji riski na kila jambo
2.	Dunia isituhadae turudi kwa Mungu	Dunia isituhadae tutakufa	Tusishughulike na mambo ya kidunia tu tutakuka na kuhukumiwa
3.	Mola tupe kheri tupate yalo mazuri	Mola tujalie kheri tupate mema	Mola tujalie tuwe waja wema tupate kufanikiwa
4.	Nia njema hairogwi	Nia nzuri hunyooka	Unapokua na Imani ya kweli utafanikiwa
5.	Mungu ni muenza wa yote	Mungu ndie mkamilifu wa yote	Mung undie mwenye uwezo wakila jambo
6.	Kazi ya Mungu haina makossa.	Kazi ya Mungu haina ubaya wowote	Lolote linalotokezea ndio apemenda Mungu liwe na hakuna ubaya
7.	Riziki haiwanywa.	Riziki haiwaniwi	Kitu kama riski yako huna haja ya kujisumbua utakipata tu
8.	Unawashukuru watu unamkufuru Mungu	Unawashukuru watu unamkosea Mungu	Unakua na Imani ya kuwategemea asiekua Mwenyezi Mungu
9.	Ewe Mola wangu ibariki ndoa yangu	Ewe Mwenyezi Mungu idumishe ndoa yangu	Ewe Mola nikinge na mabalaa
10	Jipe moyo utashinda	Jipe tamaa utashinda	Jitahidi na kumtegemea Mungu utafanikiwa
11	Alokamilika Mungu safi kiumbe hakuna	Mung undie mkamilifu	Binadamu yoyote hakosi mapungufu

Chanzo cha Data: Uwandani

4.2.2.3 Semi zilizoandikwa katika majina ya kanga Zinazohusu Bidii katika Kazi

Katika eneo hili mtafiti ameteua semi kumi na mbili na kueleza maana zake za kimsaniati na muktadha kama ilivyo kwenye jedwali na 2 hapo chini:-

Jedwali na. 4: Semi zilizoandikwa kwenye kanga zenye kuhusu Bidii katika Kazi

na	Semi	Maana zakimsamiati	Maana za kimuktadha
	Lima juani ulie kivulini	Lima kwenye muangaza wa jua ulie pasipo jua	Uhangaike kutafuta mwisho ufarijike
	Penye nia ipo njia	Penye kusudio upo usawa	Unapoweka msimamo wa kufanya kitu Mungu hukusaidia
	Mcheza kwao hutunzwa	Mcheza kwao hupewa bahashishi	Tunakiwa tutoe motisha chanya mtu anapofanya jambo zuri
	Mtarazaki hachoki	Mwenye kutafuta hachoki	Unatakiwa usikate tamaa
	Mtu ni chake	Mtu ni kitu chake	Unatakiwa ufanye kazi kwa bidi ili umiliki chako
	Mti hawendi ila kwa nyenzo	Mti haukui bila ya kuwezeshwa	Jambo lolote linahitaji atunzo
	Ukijitahidi utafanikiwa	Ukijikaza utafaulu	Ukifanya jitihada Alla atakusaidia
	Bandu bandu huishia gogo	Kidogokidogo huishia kingi	Unapofanya jambo hata kama kidogokidogo iku siku utamaliza

Jedwali na. 5 Semi zilizoandikwa katika majina ya kanga zinazohusu Maarifa

Mengineyo

1	Kaza roho umeze fupa	Kaza roho yako umeze mambo magumu	Jitahidi kwa mazito yatakayokufika
2	Lima juani ulie kivulini	Lima sehemu zenye mwangaza wa jua ulie sehemu yenye kivuli	Pata shida na tabu mwanzoni ili upate raha mwishoni
3	Hala hala ujiti na macho	Polepole ujiti na macho yako	Tahadhari na unachokifanya
4	Ukupigao ndio ukufunzao	Unaokuumiza ndio unaokupa mafundisho	Mtu hujifunza kutokana na yalomkuta
5	Bora kujikwaa dole kuliko ulimi	Bora kujikwaa katika sehemu ya mguu kuliko katika sehemu ya kinywa	Bora kufanya tatizo lolote kama kuutumia ulimi vibaya
6	Mtaka cha mvunguni sharti ainame chini	Mtaka kilicho mbali lazima atumike	Ukita kitu kizuri lazima uchakarike
7	Ndege mjanja hunasa tundu bovu	Ndege aliemjanja hunasa mara moja	Mtu mwenye tabia ya ujanja hupatikana kiurahisi
8	Kama ni wewe waweza?	Jee wewe unaweza kuyafanya hayo?	Jee una uwezo wa kuvumilia?
9	Mke hapigwi kwa fimbo	Mwanamke hapigwi kwa bakora	Mke hupambwa

Chanzo cha Data: Uwandani

4.2.2.4 Semi Zinazohusu Subira na Uvumilivu

Katika eneo hili mtafiti ameteua semi kumi na mbili na kueleza maana zake za kimsaniati na muktadha kama ilivyo kwenye jedwali na 2 hapo chini:-

Jedwali na. 6: Semi zilizoandikwa kwenye kanga zenye kuhusu Uvumilivu

Na	Semi	**Maana Ya Kimsamiati**	**Maana Ya Kimuktadha**
1	Awali si hoja bora hatima	Si bora kumaliza awali, kinachozingatiwa ni namna bora ya kumaliza	Msisitizo juu ya kulifanya jambo kwa uangalifu ili litowe matokeo bora mwishoni kuliko kuliripuaripua
2	Kaza roho umeze fupa	Jikaze mishipa ya shingo ili uweze kumeza kitu kigumu	Jitahidi kuwa na subira ilikuvumilia machungu kwa lengo la kuepusha migogoro
3	Subira ni ufunguo wa peponi	Kusubiri ni njia ya kupata pepo	Mwenye kusubiri hupata malipo mema ambayo ndiyo njia ya kumpeleka peponi
4	Mpewa hapokonyeki	Aliyepewa kitu haiwezakani kumpokonya	Aliyepewa na mungu hakuna njia ya kumkosesha alilojaaliwa
5	Sitolipiza wala sitosahau	Silipizi kisasi lakini sisahau mikasa	Japo alilofanyiwa halisahauliki lakini hapendi kulipa visasi
6	Mwenda pole hajikwai	Anaetembea kidogo kidogo hana uwezekano wa kujikwaa	Anaefanya mambo yake kwa nidhamu hufanikiwa
7	Mstahamilivu hula mbivu	Anaengojea tunda liwive basi hutarajiwa kulila lkiwa lishakuwa bivu	Mwenye kusibiri hutarajiwa kupata mafanikio kutoka kwa mungu

4.2.2.5 Semi zilizoandikwa kwenye Kanga zinazohusu Ushirikiano

Katika eneo hili mtafiti ameteua semi kumi na mbili na kueleza maana zake za kimsaniati na muktadha kama ilivyo kwenye jedwali na 2 hapo chini

Jedwali na. 7: Semi zilizoandikwa kwenye kanga zenye kuhusu Ushirikiano

na	**Semi**	**Maana zakimsamiati**	**Maana za kimuktadha**
1.	Umoja ni nguvu utengano ni uzaifu	Kuwa pamoja hujenga nguvu za mafanikio na kutengana hodhoofisha mafanikio ya watu	Inahimiza umoja na kukataza mfarakano
2.	Wingi wa mchanga ni mchanga wa funguni	Mahali penye mchanga mwingi zaidi ni funguni.	Hakuna kinachomtosha binaadamu
3.	Tuwa tugawe	Tukae pamoja tugawane kwa uwazi	Usawa wa kugawana kinachopatikamna katika rasilimali za jamii
4.	Wengi wape	Waliowengi ndio wanastahili kupewa mamlaka ya kuamua jambo.	Rai ya wengi inapaswa kuzingatiwa kuliko ya wachache. Inatundisha kuzingatia uamuzi wa jamii na kutojikita kwenye uamuzi wa washawushi wachache.
5.	Nguvu ya maji ni mawe	Maji hupata nguvu yanapoita kwenye mawe	Kitu hupata nguvu kwa kutegemea chanzo maalum kinachoweza kukisaidia. mfano mzee anapata nguvu kwa msaada wa mtoto wake n.k

4.3 Kimuktadha zinavyodhihiri kwenye Semi zenye Maudhui Mbalimbali

Mtafiti wa kazi hii baada ya kueleza maana za kimsamiati na muktadha katika semi mbalimbali aliteua baadhi ya semi hizo na kuzifafanua jinsi zinavyoendana na nadharia teule kama inavyoonekana hapo chini:-

4.3.1 Maana za Kimuktadha zinavyodhihiri kwenye Semi zenye Maudhui ya Utamaduni

Katika semi hizi thelathini, mtafiti wa kazi hii ameteuwa semi nane; takriban robo ya idadi hiyo kuonyesha jinsi maana za kimuktadha zilivyojitokeza na kuendana na nadharia teule iliyopendekezwa kutumiwa na mtafiti wa kazi hii. Usemi wa kwanza ulioiteuliwa ni ule usemao kwamba Samaki akioza usimtupe watu watakujamuokota uje ujute. Kwa mujibu wa mtafitiwa aitwae bi Mwashumu Makame Haji mwenye umri wa miaka stini na nne (64) aliyehojiwa siku ya tarehe 20/04/2018 huko Makombeni wilaya ya Mkoani mkoa wa Kusini Pemba. Makusudio hasa ya usemi huu ni kwamba “mke anapokuwa na tabia ambazo sio sahihi ni vyema kumulekeza kwanza. Kwa kufanya hivvyo huenda akaelewa na baadae akajirekebisha. Akijirekebisha maisha yataendelea. Kumuwacha kwa talaka sio suluhu ya kukimbilia utakapoumuacha anaweza kuolewa na mtu mwengine akamuelekeza akaelewa akawa mtu mwema atakaye ishi kwa insafu. Hilo likitokea muachaji wa mwanzo atabakiwa na majuto na massikitiko”.

Muktadha huu unaendana moja kwa moja na nadharia teule ya Simiotiki, ambayo kazi yake ya msingi ni kufichua dhamira zilizofichwa katika lugha ya picha na kuzidhihirisha kwa hadhira lengwa. Neno samaki limetumika kama ishara yaani lugha ya picha inayomuwakilisha mwana mke aliyeolewa na mwana mume fulani.

Neno kuoza linawakilisha ubaya na uovu wa tabia wa mke wa ndoa aliye ndani ya chuo . Neno kutupa kwa muktadha huu ni kumuacha mke kwa kumpa talaka. Hivi ndivyo nadharia ya Simiotiki ilivyotumika katika kuibua dhamira fiche iliyokusudiwa.

Nadharia hii ya Simiotiki imetoa funzo kwa jamii ya watu wa Makombeni na Wapemba kwa ujumla kwamba talaka si suluhisho la kudumu la matatizo. Kabla ya ulazima wa kutoa talaka kitakiwacho ni suluhu baina ya wanandoa. Mafunzo ya aina hii yamejaa tele kwenye mahakama za jadi vijijini, mahakama za kadhi na hata mafunzo ya vitabu vya mbinguni.

Nadharia ya maana kimatumizi na maana kimuktadha pia zimeonesha jinsi maana iliyotokana na vijenzi inavyotofautiana na maana inayofahamika katika muktadha. Msisitizo wa nadharia kimuktadha ni kwamba muktadha hupewa nafasi muhimu katika ufasiri wa maana. Maana ya usemi kupitia vijenzi vya usemi wenyewe haizingatiwi. Usemi wetu umetafsirika maana yake kwa kutumia Nadharia ya Maana Kimuktadha.

Usemi mwengine ulioandikwa kwenye kanga unaokusudiwa kuangaziwa maana yake ya kimuktadha pamoja na kuhusisha na nadharia teule ni ule usemao ***tutabanana hapa hapa.*** Kwa mujibu wa mtafitiwa bi Maryam Hilal Moh'd aliyehojiwa tarehe 22/04/2018 huko Nanguji, Kiwani, Mkoani Pemba usemi usemao tutabanana hapa hapa una maana kwamba "*vyovyote viwavyo mimi siondoki ndani ya ndoa hii hata kama tupo wengi katika ndoa hii. Wewe au nyinyi endeleeni kuwepo na mimi pia siondoki*". Wana wake wa Kipemba wengi wao wamo ndani ya maisha ya

uke wenza. Fakhari ya kila mmoja ni kutaka kupendwa dhidi ya mwenzake. Wengine hufika kufanya njama na vitimbi vya kutaka kuwang'oa wenzi wao. Basi wanawake husisitiza kwamba yeye hangoki kwa kusema ***tutabanana hapa hapa***. Uelewa huu ni ule wa kimuktadha ulioakisi moja kwa moja Nadharia ya Maana Kimuktadha na Nadharia ya Maana Kimatumizi ambazo huzingatia maana zaidi kwa muktadha wa kimatumizi kuliko kuiangalia maana kupitia vijenzi vya maneno vinavyohusika. Neno kubanana limedhihiri kwa mtazamo wa lugha ya picha inayotafsirika kwa kutumia nadharia ya Simiotiki. Kubanana kwa muktadha huu ni kubaki bila kuondoka hata kama vitimbi vitaendelea kufanywa dhidi ya mmoja miongoni mwa wengi waliochini ya mume mmoja.

Mafunzo yatokanayo na uhakiki wa usemi huu uliotafsiriwa kinadharia ni kwamba jamii inasisitozwa kulinda utamaduni wake wa uke wenza unaopendelewa kuimarika badala ya kuvunjiaka. Wanawake wa Kipemba wanatakiwa wavumiliane waendeshe maisha yao ya uke wenza na wajiepushe na vitimbi vya kutoka kung'oana kwenye mihimili yao ya uke wenza. Usemi unahimiza kila mmoja awe na msimamo wa kung'ang'ania kubaki kuliko kuwa na moyo mwepesi wa kuondoka. Mawazo haya yanaendana na mafunzo sahihi ya vitabu kutoka mbinguni.

Usemi mwengine ulioteuliwa na mtafiti kuangalia maana yake ya kimuktadha ni ule usemao kwamba ***Unapita mpakani kwangu hala hala na mbaazi zangu.*** Kwa mujibu wa bwana Mussa Moh'd Abbas aliyehojiwa na mtafiti siku ya tarehe 24/04/2018 huko Kinyasini Mkoani Pemba uesmi usemao ***Unapita mpakani kwangu hala hala na mbaazi zangu***ni "tahadhari ya bwana anaehofia wizi kotuka kwa vidume vyengine dhidi ya bibi aliyemmiliki". Anatoa thadhari ya wadowezi

waache tabia hiyo, kwani yeye hayuko tayari mkewe kuchukuliwa. Unapita mpakani maana yake unarandiarandia na mbaazi maana yake ni mke. Hayo yametafsiriwa kimuktadha kwa kutumia nadharia ya maana kimuktadha na maana kimatumizi. Neno mbaazi limejengwa kitaswira kuakisi kitu cha thamani. Maana hii fiche inaweza kutafsirika kwa kutumia Nadharia ya Simiotiki. Mbaazi kwa muktadha huu ni mke wa ndoa. Kwa maneno mengine usemi huu unaweza kujenga tafsiri isemayo usipitepite karibu na nyumba yangu kwani ninahofia huenda ukaniibia mke wangu.

Tafsiri hii iliyochambuliwa kinadharia inaonyesha tabia walionao Wapemba; wivu uliokomaa kwa upande mmoja na tabia mbaya ya kuchukuliana wake kwa upande wa pili. Usemi unaonya kwamba tabia ya kwanza ingawa inakasoro kidogo, lakini ile ya pili inalazimika kupigwa vita moja kwa moja.

Usemi wan ne ulioandikwa kwenye kanga unaohusiana na mambo ya utamaduni ambao maana yake inachambuliwa kimuktadha ni “***chunga chungio usinichunge mie si mke mwenzio”.*** Usemi huu kimuktadha kwa mujibu wa nadharia ya maana kimuktadha na maana kimatumizi unamtaka mtu ajishughulishe na mambo yanayo muhusu na kuacha kushughulika na yasiyomuhusu. Anatakiwa ajishughulishe na ya wale wanaomuhusu na aache kujishughulisha na yale ya wasio muhusu. Nadharia ya Simiotiki ambayo moja miongoni mwa kazi zake ni kufichua tafsiri zilizojificha katika lugha ya picha imefichua maana iliyokusudiwa katika chungio (ni mambo yanayomuhusu mtu) na mke mwenzio ni Yule munayehusiana kwa namna moja au nyengine.

Kwa mtazamo wa kijamii usemi unahimiza wanajamii umuhimu wa kujihusisha na mambo yanayomuhusu mtu na kuacha yale yasiyomuhusu. Kila mtu aache upekuzi usio na tija unaowahusu watu wengine ajikite kushughulikia yake nay a wengine wanaomuhusu kwa kuwasaidia na sio kuwabomoa.

Usemi mwengine ulioandikwa kwenye kanga unaoakisi mambo ya utamadumi ni ule usemao "*bora kujikwaa dole kuliko ulimi"*. Usemi huu unahimiza hadhari ya ulimi. Mtu asemaye neno lisilofaa huweza kusababisha athari kubwa na yenye maafa ya kuendelea muda mrefu sana. Athari za neno ovu ni endelevu na maafa yake ni kovu lisilopoa kwa muda mrefu. Lugha ya picha ilifananisha kujikwaa kwa viungo viwili. Kujikwaa dole kwenye maana ya msamiati na kujikwaa ulimi kunakohitaji nadharia ya Simiotiki katika kufafannua maana iliyokusudiwa. Kujikwaa ulimi ni taswiwira inayoakisi kutamka kauli isiyofaa. Basi ajikwaaye dole hupona haraka kwa kuvungwa dawa, bali ajikwaaye ulimi kwa maana ya mtamkaji neno ovu huleta athari zisizoondoka kwa haraka.

Nadharia ya Simiotiki iliyotumika kufasili taswira ya kujikwaa ulimi inaifunza jamii kuwa na hadhari katika matamko. Mwanajamii anatakiwa asitamke maneno bila kuyapima. Yanaweza kuleta dhara inayoweza kusababisha majuto makubwa kwake na pengine kwa jamii pana inayomzunguuka.

Usemi mwengine ulioandikwa kwenye kanga unaoakisi habari za kiutamadumi ni ule usemao *"hata ukinisukuma wa mbele harudi nyuma"*. Maana ya kimuktadha iliyokusudiwa kwenye usemi huu ni kwamba binaadamu mmoja hana uwezo wa kuzuwia kile ambacho mola ameamua kumpa mwenziwe. Neno kusukuma

limetumika kama lugha ya picha kusawiri maana ya kuzuia. Kwenda mbele kumetumika kuakisi mafanikio na kurudi nyuma ina akisi kuharibikiwa. Usemi unatufunza kwamba binaadamu hawezi kugeuza mafanikio ya yule aliyepangiwa kufaulu hata kama atatumia jitihada mbalimbali za kuzuia. Nadhari ya maana kimuktadha na kimatumizi zimetumika kuonyesha maana iliyokusudiwa na nadharia ya Simiotiki imetumika kufasiri lugha ya picha ya maneno “mbele” kwa maana ya mafanikio, “nyuma” kwa maana ya kuharibikiwa na “kukusuma” kwa maana ya kuzuia.

Usemi huu unaihimiza jamii kutambua kwamba hakuna haja ya kumzuia mtu juu ya riziki au chochote anachoelekea kukipata. Kufanya hivyo ni kujisumbua na kujitatiza mwenyewe. Kwani mpewa hapokonyeki.

Usemi mwengine aliougundua mtafiti wa kazi hii kwenye maandiko ya kanga ni ule usemao “*baniani mbaya lakini kiatu chake dawa”*. Kwa nadhari ya Simiotiki inayotafsiri lugha za picha mtafiti anaona kuwa baniani hapa amekusudiwa kuwa ni mtu anayefikiriwa kutokuwa na umuhimu wowote katika jamii. Pengine muovu, asiye na msaada kwenya jamii au maskini hahehohe. Lakini katika hali ya kawaida hakuna mtu asiyekuwa na faida kabisa kabisa. Anacho kitu kina manufaa. Kitu hiki kinaweza kumsaidia mwengine kwa namna moja au nyengine. Simiotiki imekiita kitun hiki kuwa ni katu. Neno dawa lina maana ya msaada ufaao kwa namna mojwapo.

Nadhari ya Simiotiki inatupa ufafanuzi kwamba watu wote katika jamii wana maana. Asiyekuwa na msada kwenye hili atakuwa na msaada kwenye jengine. Watu

wasidharauliane na kila mmoja achangie aliwezalo katika jamii na umuhimu wa kila mmoja uthaminiwe, uheshimiwe na ujaliwe.

Usemi mwengine ulioteuliwa na mtafiti kuangalia maana yake ya kimuktadha ni ule usemao kwamba “namuogopa simba kwa meno yake simuogopi mtu kwa maneno yake”. Simba na meno yake ni mtu mwenye nguvu na uluwa wa kuweza kumsababishia mwengine madhara. Mtu huyu ni yule mwenye cheo na madaraka ambaya huweza kutoa amri tu ya kusababisha mwengine kuadhibiwa na mtu na maneno yake ni mtu wa kawaida ambaye hana dhara wala kitisho chochote dhidi ya mwengine. Tafsiri hii inatokana na nadharia ya maana kimuktadha na maana kimatumizi juu ya usemi teule. Usemi huu unatuonyesha kwamba jamii ya Wapemba hushtushwa na wenye vyeo na wenye sauti na kuona ni kawaida tu kubishana na watu wasio na hadhi au mamlaka yoyote.

4.3.2 Maana za Kimuktadha zinavyodhihiri kwenye Semi zenye Maudhui ya Imani na Dini

Katika semi kumi na tano zilizoainishwa na mtafiti wa kazi hii ameteua semi tano takriban thuluthi ya idadi hiyo kuonyesha jinsi maana za kimuktadha zilivyojitokeza na kuendana na nadharia teule iliyopendekezwa kutumiwa na mtafiti wa kazi hii.

Usemi wa kwanza ulioteuliwa na kuangaziwa maana yake ya kimuktadha ni ule usemao *“mpaji ni Mungu”*. Usemi huu uko bayana kabisa kuonyesha kiwango cha imani cha jamii ya Wapemba. Kwa utamaduni na imani yao ya Kidini kila akipatacho mtu huwa amekipata kwa uaamuzi wa Mungu. Hivyo wanajamii huutumia usemi huu kuonyesha kuridhika kwa yule aliyekosa na kuonyesha shukrani

kwa aliyepata. Aliyekosa huamini kwamba Mungu hajaamua kumpa, akiamua nay eye atampa tu. Aliyepata hukiri kwamba kapata kutoka kwa Mungu. Muktadha huu ndio uliodhihiri kwenye matumizi ya maana kimuktadha na maana kinadharia.

Usemi unaelekeza kuwacha kuoneana choyo kwani aliyepewa kapewa na Mungu aliyekosa kakoseshwa na Mungu. Semi inatufunza kuwa hakuna haja ya kulalamilka kwa aliyekosa, kwani aliyekosa pia kakoseshwa na Mungu. Kila mmoja anapaswa amuombe na amtegemee Mungu.

Usemi mwengine wa kundi hili ambao mtafiti aliamua kuangazia maana yake ya kimuktadha ni “nia njema hairogwi”. Kuroga ni kutumia mbinu za jiza kwa lengo la kuharibu ufanisi wa maendeleo ya mwengine. Mbinu hizo ni pamoja na ushirikina, uchawi, usihiri na njia nyenginezo za aina hiyo. Hapa neno kuroga limetafsiriwa kimuktadha kama kumkalia vibaya yule unaeishi nae. Nia ya mmoja inakuwa haina ukorofi wa aina yoyote, lakini mwengine anakuwa na nia ovu. Mara nyingi huyu mwenye nia ovu huharibikiwa na mwenye nia njema huonyesha kutambua uovu wa mwenzake kwa kusema nia njema hairogwi. Nadharia ya Simiotiki inatafsiri lugha ya picha “kuroga” kwa maana ya kukaliana vibaya na kuonyesha yule aliyekaa vibaya kwa mwenzake ndiye aharibikiwaye na aliyekaa vyema hutengenekewa kwani nia yake huwa hairogeki.

Usemi unatufunza kwamba ni jambo linalokatazwa watu kukaliana visivyo. Kila mmoja anapaswa kutakasa nia juu ya mwenzake na muovu wa nia si aghlabu kufanikiwa katika jambo lake.

Usemi wa tatu ambao mtafiti aliamua kuangazia maana yake ya kimuktadha ni ule usemao “Kazi ya Mungu haina makosa”. Mtafiti wa kazi hii siku ya tarehe 28/4/2018 alihojiana na bwana Bakari Rajab Mbwana ili kupata maana ya usemi huu uliojitokeza katika kanga. Alisema kwamba maana ya usemi huu ni kwamba Alla hufanya atakalo bila kujali athari ya jambo hilo kwa waja wake. Uamuzi wa Alla haushitakiwi na wala haupingiki. Hutokana na makadirio na matakwa yake. Kutokana na jambo hilo wanaadamu hupaswa kupokea hata kama kulipokea kunakuwa na uchungu mkali baadhi ya muda. Kuonesha kiwango cha kukosa kwao hiari hujisogeza kwa Mungu na kujieleza kwamba wameridhia uamuzi wa Alla, kwa kusema hii ni kazi ya Mungu na kazi ya Mungu haina makosa. Maana yake ya kimuktadha iko wazi kabisa na ni usemi unaotumika kumtaka Mja aridhie uamuzi wa Mungu kwani hana budi nao.

Jamii ya watu wa Pemba inaonekana kwa kiasi kikubwa huyarejesha matukio yote kwa muumba wao. Makubwa, madogo, yanayofurahisha, yanayokera na yote yanayowafika. Na kwa kuwa Mungu keshaamua ndo keshaamua na uamuzi wake hauhukumiwi na mtu. Usemi huu aghlabu/mara nyigi hutumika kumliwaza mtu aliyefikwa na janga, maafa au msiba. Na mara nyengine Yule aliyefikwa hujiliwaza mwenyewe kwa kutamka usemi huu.

Usemi wa nne kwenye eneo hili ulioteuliwa na mtafiti kubainisha maana yake ya muktadha kwenye kazi hii ni “Machozi ya Mnyonge malipo kwa Mungu”. Mzee mmoja mtu mzima wa miaka kama sabiini (70) aitwae Fatma Khamis Kumbaro ailhojiana na mtafiti juu ya usemi huu. Mahojiano yao yalitokea siku ya tarehe 30/4/2018 huko Makombeni mkoa wa kusini Pemba. Mzee alisema kwamba maana

ya mnyonge hapa ni mtu anayevumilia shida kwa kudhulumiwa au sababu nyengine. Amekosa msaada kwa watu. Wake yeye ni Mungu tu. Malipo yote anayategemea na kuyatarajia kutoka kwa Mungu. Machozi ni yale mashataka na malalamiko anayoyatoa kwa kumuomba Mungu amlipie." Maana hii iliyotolewa ni ya kimuktadha inayoendana na nadharia teule za Simiotiki na maana Kimuktadha na maana Kimatumizi. Simiotiki imetumika kufumbua fumbo lisemalo Machozi ya mnyonge na nadhari nyenzake zimeonesha maana iliyokusudiwa kwa ujumla.

Usemi huu kimatumizi katika jamii hutumika kumpa moyo aliyekoseshwa haki na watu atarajiye kuipata haki hiyo ingawa si hapa duniani, lakini itapatikana kwenye utukufu wa Mungu. Hivyo asivunjike moyo, aendelee kusibirin tu. Mtafiti anasisitiza kwamba haina maana kwamba mtu asidai haki yake, ila anaposhindwa ajuwe kwamba mlipaji wa kumlipia yupo.

"Alokamilka Mungu Safi kiumbe hakuna" ni usemi mwengine alioupata mtafiti wa kazi hii kwenye maandishi ya kanga. Alipofatilia maana yake aliambiwa usemi huu unaonyesha uwezo wa Allan a ukamilifu wake. Pia kwa upande mwengine unaonesha udhaifu na kasoro za kiumbe nmwanaadamu. Kila mtu anakasoro zake. Kimuktadha usemi huu hutumika kukubali na kuridhia kosa lililotendeka kutoka kwa mtu fulani. Pia hutumika kupunguza kibri cha ajionae fundi mkubwa wa fani fulani fulani.

Jamii huutumia usemi huu kumtukuza mola wao sambamba na itikadi ya dini yao na pia hutumika kuonyesha upunguku wa kiumbe mtu vyovyote awavyo.

4.3.3 Maana za Kimuktadha zinavyodhihiri kwenye Semi zenye Maudhui zinazohusiana na Maarifa Mbali Mbali

Katika semi kumi zilizoainishwa na mtafiti wa kazi hii kwenye kipengele hiki ameteua semi tatu takriban thuluthi moja ya idadi iliyotajwa hapo juu kuonyesha jinsi maana za kimuktadha zilivyojitokeza na kuendana na nadharia teule iliyopendekezwa kutumiwa na mtafiti wa kazi hii.

Usemi wa kwanza katika hizo tatu ni “kikulacho kinguoni mwako”. Nadharia ya Simiotiki imetumika kufasiri usemi huu kwa ujumla wake. Kikulacho imefasiriwa kwa maana ya mtu anayekufanyia uadui au hasadi ya aina nyengine. Nguoni mwako ni ukaribu ulio mkubwa kabisa baina ya mtu na mtu. Ukaribu wa nguo na mvaaji wake ni mfano hai uliopigwa kuonyesha mahusiano ya adui na afanyiwae uadui. Kimuktadha usemi huu hutumika kuonyesha kwamba adui wa mtu yawezekana akawa ndugu yake wa damu, au mtu wa karibu anayemjua nje ndani, ndani nje. Uchambuzi huu ni kwa mujibu wa bi Mwashum ambaye ni kiongozi wa serikali ya mtaa/sheha huko Makombeni aliyehojiwa siku ya tarehe 02/05/2018.

Katika jamii usemi huu hutoa tahadhari kumjulisha kuwa uadui afanyiwawo unafanywa na mtu si wa mbali. Bala ya kutumia maelezo mengi Waswahili husema “kikulacho kinguoni mwako”.

Usemi wa pili katika hizo tatu ni “ mtaka cha mvunguni sharti ainame chini” . Usemi unahimiza juhudi isiyompaka katika kutafuta jambo. Haya ndiyo yajulikanayo na jamii. Maneno hayo mtafiti aliyapata kutoka kwa mtafitiwa wake bi Fatma Khamis Kumbaro siku ya tarehe 30/04/2018. Mvungu na kuinama zimetafsiriwa kisimiotiki.

Mvungu inawakilisha jambo lipatikanalo kwa mashaka makubwa sana na kuinama inawakilisha juhudi ya hali ya juu. Kwa muktadha huo “ mtaka cha mvunguni sharti ainame chini” ina maana mtaka jambo gumu sana kupatikana sharti afanye jitihada ya juu, kinyume chake atashindwa.

Usemi wa tatu katika hizo ni “ mke hapigwi kwa fimbo”. Kwa mujibu wa mzee mmoja aitwae bwana Faki usemi huu una maana kwamba mke anapaswa kutunzwa na kutafutiwa mahitaji ya kujipamba na kujiremba. Hiyo ndiyo fimbo yake inayomtuliza na kumpa heshima ya kutulia kwa mumewe. Kumpiga kwa pigo la kawaida haijengi nidhamu ya kweli. Kinachojenga nidhamu ya kweli ni huduma zilizotimia. Baadhi ya wanaume huwajenga wake zao kwa nidhamu za woga ambazo hazina tija.Kinachojenga heshima ni ukamilfu wa huduma za ndani na sio makofi na magongo. Hii ndiyo maana ya kimuktadha ya usemi huu. Nadharia ya Simiotiki imetumika kuzifananisha huduma sahihi na mapigo ya mke. Jamii huitumia semi hii ili kuwahadharisha wanaume kuacha kuwatesa wake zao kwa dhana ya kujenga nidhamu. Usemi unahimiza huduma sahihi katika maisha ya ndoa.

4.3.4 Maana za Kimuktadha zinavyodhihiri kwenye Semi zenye Maudhui zinazohusiana na Bidii katika Kazi

Katika semi kumi zilizoainishwa na mtafiti wa kazi hii kwenye kipengele hiki ameteua semi tatu takriban thuluthi moja ya idadi iliyotajwa hapo juu kuonyesha jinsi maana za kimuktadha zilivyojitokeza na kuendana na nadharia teule iliyopendekezwa kutumiwa na mtafiti wa kazi hii.

“Usemi wa kwanza ni ule usemao mcheza kwao hutunzwa. Kwa kuangalia muktadha wa kimatumizi methali hii imetafsiriwa kwa mtazamo kwamba “***ni wajibu wa wanajamii wa eneo fulani kumuenzi na kumtunza mtu wao aliyewafanyia jambo bora na la thamanii.”*** Kama pana natija ya malipo alipwe vyema kwa kiasi cha kuridhisha, ajaliwe, athaminiwe na aheshimiwe. Huu ndiyo muktadha wa kimatumizi uliokusudiwa. Usemi huu unaihimiza jamii kutunzo hazina zake, wakiwemo watu bora wanaoitumikia jamii hiyo. Usemi mwengine uliokusanywa na mtafiti wa kazi hii ni ule usemao “*Mtarazaki hachoki*”. Kimuktdaha usemi huu unatumika kuonyesha kwamba, ingawa riziki inatoka kwa Mungu, lakini mwenye kuitafuta anatakiwa atumie bidii kubwa bila kuchoka, kwani atakapochoka na kubaki bila kufanya kazi maisha huenda yakamcheza kwani riziki haiji bila sababu. Usemi unaihimiza jamii umuhimu wa kufanya kazi. Unaitaka ifanye bila kuzembea wala kuchoka. Usemi wa tatu ulioteuliwa na mtafiti wa kazi hii ni kwenye kipengele hiki ni “Jembe halimtupi mtu”. Jembe katika usemi huu limetumika kuashiria kilimo. Hii ni kwa mujibu wa mtafiti wa kazi hii huku akiongozwa na “Nadharia ya Simiotiki”, ambayo moja miongoni mwa mihimili yake ni kufumbua fumbo na fumbizi zilizowasilishwa kwa lugha ya taswira na ishara. Kimuktadha usemi huu una maana kwamba, kilimo hakiwezi kumuangusha mkulima. Anaelima bila shaka atafaidika na kilimo chake. Iwe kwa kupata mzao ya chakula, au kupata fedha kwa kuuza ziada ya mazao yake au pengine kwa kuuza mazao maalum ya biashara.

Usemi huu unaikumbusha jamii umuhimu wa kilimo na kwamba kilimo si kazi ovyo, lakini ni kilimo chenye natija kubwa mno. Ni muhimu watu kukishughulikia na kukipa hadhi.

4.3.5 Maana za Kimuktadha zinavyodhihiri kwenye Semi zenye Maudhui zinazohusiana na Subira na Uvumilivu

Katika semi kumi zilizoainishwa na mtafiti wa kazi hii kwenye kipengele cha Subira na Uvumilivu ameteua semi tatu takriban thuluthi moja ya idadi iliyotajwa hapo juu kuonyesha jinsi maana za kimuktadha zilivyojitokeza na kuendana na nadharia teule iliyopendekezwa kutumiwa na mtafiti wa kazi hii. “Nimeonesha busara mbona sasa mwanikera”. Usemi huu mtafiti baada ya kuudondoa kwenye vazi la kanga alitaka kuelewa hasa umekusudiwa nini? Alimfuata bi Maryam Sharif wa Makombeni mkoa wa Kusini Pemba ili kutafuta maana iliyokusudiwa. Bi Maryam alisema, usemi unaelekeza kwamba mtu alieonesha ustahamilivu ni bora kuachiwa na shughuli zake. Hakuna haja ya kulazimishwa kuingia kwenye malumbano yasiyo ya lazima. Usemi unatufunza kwamba wanajamii wanatakiwa wawe na utamaduni wa kuvumiliana na kusamehe baadhi ya vitu. Wanapoingia kwenye mizozo waimalize mizozo yao kwa njia za busara kubwa. Na suluhu ikeshapatikana hakuna haja ya kukumbusha maswali yaliyosababisha matatizo.

Usemi wa pili uliochukuliwa katika eneo hili ni “kaza roho umeze fupa”. Lugha iliyotumika hapa ni ya ishara, fupa linawasilisha shida na makero yanayothakili moyo wa mwanaadamu. Kwa hivyo kaza roho umeze fupa inamtaka mtu akabiliane na ghamidha zinazomthakili astahamili, avumilie na asamehe mengi yanayotokea ili kuepusha mizozo na migogro katika jamii. Wanajamii wanapaswa wawe wastahamilivu, wavumilane na kusameheana. Wakifanya hivyo wataepesha migogoro na mivutano na chuki baina yao.

“Subira ni ufunguo wa Peponi”. Subira ni ni uvumilivu, uvumilivu kwa mujibu wa mafunzo ya vitabu vya mbinguni ni katika kheri kubwa inayoweza kumpatia muunini malipo makubwa kutoka kwa mola wake. “Ambao hutoa(katika hali) ya wasaa na(katika hali) ya dhiki, na wazuiao ghadhabu na wanasamehe watu (na wawafanyiao ihsani), na Mwenyeezi anawapenda wafanyao ihsani (Quran 3:134). Kwa mujibu wa imani za kidini mtu anatakiwa awe anpenda kustahamili na kusubiri ili alipwe mema ana apate ukaribu na Mungu huko Mbinguni.

4.3.6 Maana za Kimuktadha zinavyodhihiri kwenye Semi zenye Maudhui ya Ushirikiano

Katika semi tano zilizoainishwa na mtafiti wa kazi hii a usemi mmoja umeteuliwa kuonyesha jinsi maana za kimuktadha zilivyojitokeza na kuendana na nadharia teule ziliyopendekezwa kutumiwa na mtafiti wa kazi hii. Usemi aliouteuwa ni ule usemao kwamba “umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu”. Neno umoja kwenye usemi huu limewekwa kutafsiri nguvu na neno utengano limefasiri udhaifu. Tafsiri hii ni kwa mujibu wa nadharia ya Simiotiki itumikayo kuchambua lugha ya ishara katika maneno ya lugha au semi za kifasihi. Usemi huu unatumika kimuktadha katika jamii kuhimiza watu kushirikiana na kuwa wamoja na kuacha kutengana kwani iwapo watu watafanya mambo kwa pamoja, jambo lao hupata nguvu na iwapo kila mmoja anajifanyia peke yake, jambo lao litadhoofika na kukosa baraka. Ili watu kwa mfano wanafamilia wanatakiwa wawe pamoja na washirikiane huambiwa jamani umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu.

4.4 Hitimkisho

Sura hii mimewasilisha na kubainisha uchambuzi wa data kutegemeana na malengo yaliyowekwa. Kuhusu lengo la kwanza mtafiti aliorodhesha semi zilizohusika na kada tofauti tofauti. Semi zilizobainishwa ni zile zinazohusiana na dini na imani, zinazohusu maarifa ya jumla, bidii ya kazi katika jamii, ushirikiana na subira na uvumilivu. Lengo la pili liliwasilisha maana za semi za kimsamiati na kimuktadha. Lengo la tatu na la mwisho linafafanuwa na kuchambua maana za kimuktadha na jinsi zinavyoakisi jamii ya Wapemba.

SURA YATANO

MUHTASARI WA UTAFITI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Sura hii ni sura ya mwisho ambayo inatoa Muhtasari, Hitimisho na Mapendekezo ya utafiti huu. Sura hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu ambazo ni: Sehemu ya Muhtasari, sehemu ya Hitimisho na sehemu ya Mapendekezo ya utafiti.

5.2 Muhtasari

Utafiti huu ulihusu mada ya utafiti isemayo: ***Maana za kimuktadha zilizojitokeza katika semi zilizoandikwa katika majina ya kanga.*** Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni: Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza maana za muktadha zilizojitokeza katika semi zilizoandikwa katika kanga. Malengo mahsusi yalikuwa matatu ambayo: Kubainisha semi mbali mbali zilizoandikwa katika kanga. Kubainisha maana za kimsamiati za semi teule zilizoandikwa kwenye kanga. Kuchambua maana za muktadha za semi teule zilizoandikwa kwenye kanga.

Hivyo basi, kutokana na malengo mahususi haya, utafiti huu uliongozwa na maswali matatu ya utafiti yafuatayo: i) Ni semi gani ambazo hujitokeza katika majina ya kanga? ii) Ni maana zipi za kimsamiati hupatikana katika semi teule zilizoandikwa katika kanga? iii) Ni zipi maana za kimuktadha zinazopatikana katika semi teule zilizoandikwa kwenye kanga? Utafiti huu una sura tano zifuatazo: Sura ya kwanza ilihusu Utangulizi wa jumla. Vipengele vya kiutangulizi vilivyojadiliwa katika sura hii ni utangulizi, usuli wa mada, tatizo la utafiti, Malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, muundo wa tasnifu. Sura ya pili ilihusu Mapitio ya Kazi Tangulizi na Mkabala wa Kinadharia. Sura ya tatu imejadili na kufafanua mbinu za

utafiti. Sura ya nne ilihusu Uchambuzi na Uchanganuzi wa data za utafiti. Sura ya tano ilikuwa zaidi inahusu Muhtasari wa Utafiti, Hitimisho na Mapendekezo. Data za utafiti huu zilichambuliwa kwa njia ya maelezo kwa kutumia nadharia tatu tofauti. Nadharia hizo ni nadharia ya Maana Kimatumizi, nadharia ya Maana Kimuktadha pamoja na Nadharia ya Simiotiki.

5.2.1 Lengo Mahsusi La Kwanza

Lengo mahsusi la kwanza la Utafiti huu lilikuwa ni: Kubainisha semi mbali mbali zilizoandikwa katika kanga. Lengo hili liliongozwa na swali la msingi la kwanza lisemalo: Ni semi gani ambazo hujitokeza katika majina ya kanga? Matokeo ya utafiti huu yalionesha kuwa kuna semi mbalimbali zilizotofautiana kimaudhui ambazo zimeandikwa katika kanga. Semi hizo zimejikita katika maudhui za mila na utamaduni wa jamii, dini na imani, maarifa mengineyo, bidii katika kazi na subirá na uvumilivu.

5.2.2 Lengo Mahsusi la Pili

Lengo mahsusi la pili la utafiti huu lilikuwa ni: Kubainisha maana za semi teule zilizoandikwa kwenye kanga. Lengo hili liliongozwa na swali lisemalo: Ni maana zipi hupatikana katika semi teule zilizoandikwa katika kanga*?* Matokeo ya utafiti huu yalionesha kuwa maana za semi zinajikita kimsamiati na kimuktdha. Maana za kimsamiati huibuka kutokana na vijenzi mahususi vilivyojenga usemi wenyewe. Maana za kimuktadha zinatokana na tafsiri mahususi inayotokana na mtazamo na muktadha wa kimatumizi kama inavyofahamika na jamii husika.

5.2.3 Lengo Mahsusi la Tatu

Lengo mahsusi la tatu la utafiti huu ni: Kuchambua maana za muktadha za semi teule zilizoandikwa kwenye kanga. Lengo hilo liliongozwa na swali la tatu la utafiti lisemalo kwamba Ni zipi maana za kimuktadha zinazopatikana katika semi teule zilizoandikwa kwenye kanga.

Katika utafiti huu, mtafiti amegundua kuwa semi zilizo katika maudhui mbalimbali huandikwa kwenye kanga ili kufikisha ujumbe maalum kwenye jamii ambapo kanga huvaliwa. Semi hizo kukanya, hukosoa na hata kuelekeza juu ya utendaji bora wa mambo katika jamii husika. Kwa mfano maswali ya wivu uliokomaa ulizungumziwa, umuhimu wa kubaki kwenye ndoa, umuhimu wa kuheshimiana, umuhimu wa bidii ya kazi, subirá na uvumilivu na maadili kadha ya kijamii yalihusishwa kwenye lengo hili la tatu.

5.3 Hitimisho

Kwa kuhitimishia, tunaweza kusema kwamba semi za Kiswahili, zilizoandikwa kwenye kanga zikiwemo zinajidhihirisha kwa maneno ya kawaida, lakini unazingatiwa zaidi ni muktadha wake wa kimatumizi kuliko ile maana iliyodhihiri kwenye vijenzi vya usemi wenyewe.

5.3.1 Utoshelevu wa Nadharia

Nadharia zilizotumika katika uchambuzi na uwasilishaji wa data katika utafiti huu ni Nadharia ya maana ya matumizi na Nadharia ya maana ya muktadha pamoja na Nadharia ya Simiotiki.. Kupitia nadharia hizo mtafiti aliweza kuchambuwa na kuwasilisha dhamira zilizojitokeza katika semi zilizoandikwa katika majina ya kanga. Nadharia ya maana kimuktadha ilitumika kutoa ufafanuzi, hasa katika kueleza

maana iliyokusudiwa kwenye usemi husika, bila kujali aina ya maneno au vijenzi vilivyojenga semi hizo. Nadharia ya Simiotiki imetumika kufumbua fumbo na fumbizi zilizofinyanga maana lengwa iliyomo katika usemi.. Kwa hivyo nadharia teule zimeweza kusaidia kuzichunguza semi mbalimbali za majina ya kanga katika jamii ya Kipemba kulingana na shughuli zao mbalimbali za kimaisha pamoja na mila zao, silka zao, utamaduni wao, uchumi wao nakadhalika. Hatimaye kubainisha kwa uwazi malengo ya utafiti huu kama yalivyotarajiwa na mtafiti wa utafiti huu uliofanyika.

5.4 Mapendekezo ya Utafiti

Kutokana na matokeo ya tasnifu hii baada ya kukamilika, maoni na mapendekezo yafuatayo yanatolewa; Pamoja na umuhimu wa kufahamu maana za muktadha katika semi zilizoandikwa kwenye majina ya kanga, serikali inashauriwa kwa kutumia vyombo na taasisi zake mbalimbali, ikiwemo Wizara ya Elimu na Ufundi kwa Tanzania Bara na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa Tanzania visiwani, kudumisha matumizi ya semi zinazopatikana katika kanga kwa kuongeza vipindi vya masomo katika mitaala na kuisimamia ipasavyo. Kwa maana hiyo watunzi na wataalamu mbalimbali wa fasihi wanashauriwa kuzikusanya na kuzichambua semi kwa kina ili waweze kuwafaidisha watu wengi. Vyombo vya habari kama vile redio na TV vinashauriwa kuongeza vipindi vya fasihi simulizi ikiwemo semi. Magazeti na majarida yaanzishe makala mbalimbali ili semi zilizoandikwa katika kanga , ziweze kupata nafasi kubwa zaidi ya matumizi. Mtafiti pia, anapendekeza kwa jamii hasa wazee kujenga mazingira ya kukaa pamoja na vijana ili kuwafahamisha umuhimu wa asasi hii muhimu ya semi katika maisha yao.

5.4.1 Mapendekezo kwa Tafiti Zijazo

Kwa vile utafiti huu umefanyika katika kisiwa cha Pemba tu, na Zanzibar ni visiwa viwili yaani Pemba na Unguja, ni vyema kabisa tafiti zijazo zifanyike katika kisiwa cha pili cha Unguja, ili kuweza kupata idadi kubwa zaidi ya semi zilizoandikwa katika majina ya kanga . Semi hizo zinazohifadhiwa kwa ajili ya kizazi cha sasa na kizazi kitakachokuja baadae**.** Pia mtafiti wa kazi hii anashauri mbinu za kiisimu zitumike katika kuchambua semi za aina nyengine za kifasihi. Mifano ya semi hizo ni kama vile semi zilizoandikwa kwenye mikoba, makawa na vyanzo vyengine.

MAREJELEO

Alhabib, E. (2012). *Matumizi ya lugha katika Nyimbo za Taarab*. Tasnif ya M.A Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Babbie, E. (1999). *The Basics of Social Research*, Belmont. Wadisworth Publishing Company.

Best, W. R. and Gall, M. (1996). *Educational Research An Introduction*. New York. Longman.

Bodunrin, P. (1981). "*The Question of African Philosophy* "*in Philosophy*; America 1984. The Journal of the Royal Institute of Philosophy University Press.

Chuachua, R. (2011). *Itikadi katika riwaya za Shaaban Robert*. Taasisiya Taaluma za Kiswahili. Chuo kikuu cha Dar es salaam.

Enon, J. C. (1998). *Educational Reseach; Statistics and Measurement.* Kampala, Makerere University.

Finnegan, R. (1979). *Oral literature in Africa*. Nairobi, Oxford University Press.

Hamad, A. K. (1981) *Tanzu za Fasihi Simulizi; Misingi ya Nadharia ya Fasihi*. Zanzibar, TAKILUKI.

Hassan, A.U. (2013). *Dhima ya Methali katika jamii ya Wapemba*. Chuo kikuu cha UDOM.

Khatib, M. S. (1978). *Vitendawili Fani ya Fasihi Simulizi* Mulika NO.13. Dar-es-salaam, TUKI

Kothari, C. R. (2008). *Research Methodology; Methods and Techniques*. New Delhi. New Age International Publishing Ltd.

Mahaveer, S. and Udaiveer, S. (2010). *Philosophical Foundation of Education*. Laxmic Publication Pvt. Ltd.

Mahenge (2009) *Semi zitumikazo kwenye tiketi za daladala* katika Mulika namba 29na 30 TATAKI.

Matinde R.S (2012) *Dafina ya Lugha Isimu na Nadharia .Kwa Sekondari vyuo vy kati na vyuo Vikuu.*Educational Publishers (T)Ltd.

Mauya B,A (2006) *Semi maana na matumizi* Chuo Kikuu cha Dar –es-salam TUKI.

Ministry of Education Zanzibar (1997). *Environmental Studies.* Zanzibar, Printed by Alkhayria Press.

Mnata. R.(2014) *Semantiki na Pragmatiki ya Kiswahili* Dodoma Tanzania.

Mulokozi MM (1989) *Tanzu za Fasihi Simulizi* Mulika 21,1-24,Dar es salaamTanzania Publishing House.

Mulokozi, M. M. na Kahigi, K. K. (1979). *Kunga za ushairi na Diwani Yetu*. Dar es Salaam, Tanzania Publishing House.

Mulokozi,M,M (1996) *Fasihi ya Kiswahili* Chuo Kikuu Huria Cha Dar –es-salamu.

Nassor.H.J (2016) *Semi zilizoandikwa kwenye vyombo vya safari vyaa Baharini Kisiwani Pemba*. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania .

Ndungo C.M na Wafula , R.M (1993) *Tanzu za Fasihi Simulizi*.Unirsity of Nairobi

Omari, C. K. na Mvungi, M. (1981). *Urithi wa Utamaduni wetu*. Dar-es-salaam, Tanzania Publishing House.

R. Kaduguda ,.J. Kiango na T. Ipara (2015) *Kiswahili Shule za Sekondari Kidato cha kwanza* .

Robinson, D. and Groves, J. (2004). *Introducing Philosophy*. Published in the UK in 2004 by Icon Books Ltd

Sengo T.S.Y.M (2009) *Sengo na fasihi za kinchi* Dar es salaam .AERA Kiswahiki Research Products.

Senkoro, F. E. M. K. (2011). *Fasihi*. Dar-es-salaam: KAUTTU.

Taasisi ya uchunguzi wa kiswahili, (2004). *Kiswahili*. Chuo Kikuucha Dar-es-salaam Tanzania, TUKI.

TAKILUKI (1981). *Misingi ya Nadharia ya Fasihi*. Printed in Sweden by Berlings Arlov.

Uledi, F.M *Muundo wa Lugha katika Methali na Vitendawili kwa jamii ya Wamakunduchi.* (2012) Wilaya ya Kusini Unguja. Chuo Kikuu Cha UDOM.

TUKI (2009), *Kamusi la Kiswahili*, DSM, Dar-es-Salaam, University Press

Walliman, N. (2005*). Your Research Project 2nd Edition*, London, SACE Publication Ltd.

Wamitila, K. W. (2004). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Focus Publication Limited.

Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi, Misingi ya vipengele vyake*. Nairobi, Phoenix Publishers Ltd.

Wamitila.K.W.(2013) *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*,Focus Publications Ltd Nairobi.

Wanjala.F.Simiyu (2013) *Kitivo cha Fasihi Simulizi kwa Shule na Vyuo na Ndaki* . Chuo Kikuu cha Kenya Nairobi.

VIAMBATANISHO

Kiambatanisho Na 1: Hojaji kwa wazee kati YA MIAKA (60-80) na vijana kati ya miaka (18-39) NA WATU MAKAMO (40-59)

SEHEMU A: Maelezo binafsi ya muhojiwa

1. Umri wako ……..
2. Mume……Mke……
3. Unapoishi……..
4. Kazi unayofanya……

SEHEMU B: Mahojiano kuhusu Mada

1. Je unazifahamu semi?
2. Unaweza kunitajia semi zinazopatikana kupitia majina ya kanga.
3. Je semi hizo ulizonitajia unaweza kuniambia maana halisi za semi hizo?
4. Jee unaweza kunieleza maana ya ndani ya semi hio iliokusudiwa kwa jamii?
5. Una maomi gani kwa watumiaji wa kanga zenye semi mbali katika jamii ya wapemba.

Ahsante sana kwa msaada wako mzuri

Kiambatanisho Na 2: Hojaji kwa wafanya biashaRA wa vazi la kanga;

Sehemu A: Maelezo binafsi ya muhojiwa

1. Umri wako……..
2. Mume……Mke……
3. Unapoishi…….
4. Kiwango cha elimu…….

SEHEMU B: Mahijiano kuhusu mada

1. Nitajie semi angalau tatu zinazopatikana na kupendwa na wateja wa vazi hili?
2. Je unaweza kunitajia maana ya semi hizi kulingana na uhitaji wa wateja wako?
3. Naomba unipe maana lengwa kwa wateja wanaotumia kanga pendwa zenye semi hizi kutoa ujumbe kwa jamii.

Ahsante sana kwa msaada wako mzuri

Kiambatanisho Na 3: SEMI ZILIZOANDIKWA KWENYE KANGA ZENYE MTAZAMO WA KIUTAMADUNI

1. Huruma si malezi
2. Lishalovuusha gogo
3. Bora kukatwa na bati kama kukosa bahati
4. Vicheko vyenu chekeni yangu niwachieni
5. Nalala nijipumzishe mafisadi wasinishughulishe
6. Nikiwepo hamunienzi na kunikosa hamuwezi
7. Nikiwepo nawa mwema nikiondoka mwanisema
8. Kuolewa ni sharia kuzaa ni majaaliwa
9. Wastara hasumbuki
10. Sitolipiza wala sitosahau
11. Muyaseme kwa udhati kusingiziwa sitaki
12. Usinitafute undani siri yako iko ndani
13. Likinifika nitakujibu
14. Mgonjwa tumpe pole muongo tumpe nini?
15. Tabia imenipendeza
16. Mimi ni mwalimu wako na huko kujua kwako
17. Nitaishi naekwa raha na tabu
18. Mwisho wa kuranda utarejea
19. Mwenye wivu ajinyonge
20. Bwana nipe wiki kazi na njaa haifanyiki
21. Hajinyongi mtu hapa

22. Kinyago cha mpapure nyamaza nikusitiri
23. Utabanana na nani nawe mchafu
24. Kila uonalo wasema na hili pia kaseme
25. Ukiwa tapeli maisha yako yatafeli
26. Ujirani naupenda lakini tabia zimenishinda
27. Moyo wangu tuwa kila kitu ni hatua
28. Usijirahisi nafasi niyako
29. Wivu ni kidonda ukishiriki utakonda

Kiambatanisho Na 4: SEMI ZILIZOANDIKWA KWENYE KANGA ZENYE DINI NA IMANI

1. Apendalo Mola huwa.
2. Dunia mapito
3. Mstahamilivu hula mbivu.
4. Subira ufunguo wa peponi
5. Safi nia upate kutulia
6. Safari sio kifo
7. Mshukuruni Mungu kwa kila jambo
8. Zina Mola riziki
9. Yailahi ya Karim mstiri mja wako
10. Maisha matamu lakini mafupi
11. Palipo na upendo Mungu yupo
12. Mema nakutakia na kheri nakuombea
13. Naomba rabi salama
14. Mungu ndie mbariki ndie mtoaji riziki
15. Hayawi hayawi huwa
16. Ndoa ni jambo la kheri Mungu hulibariki

17. Nyumba yenye upendo haikosi riziki

18. Yarabi tunusuru midomo ya watu isituzuru

19. Jihadhari nayo dunia mti mkavu

20. Kila jambo hupangwa na Mungu

21. Kila mtenda mema Mungu humpa wema

22. Riziki ya mtu hupangwa na Mungu

23. Tukimuomba Mungu nuru itashuka

24. Tumshukuru Mungu kwa kila jambo